# Nipashe

Jumamosi Juni 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580251

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Takukuru yaokoa mil. 241.3/- Afya Saccos, yarejeshea wanachama, wastaafu

UKURASA 3




UKURASA 11



# MAGUFULI: HAKUNA CORONA

**ASEMA** ugonjwa umepungua na ana uhakika utaisha, Tanzania ilianza na Mungu na itamaliza...

*Endelea ukurasa 2*

Rais John Pombe Magufuli, akizungumza wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), katika uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## BAA LA CORONA



Upimaji wa joto wakati wa kuingia au kutoka kwenye eneo la mkusanyiko wa watu, haumaanishi kuzuia maambukizo kutoka kwa mtu ambaye ameambukizwa virusi vya corona kwenda kwa mwingine, anaweza kuwa bado yuko kwenye kipindi cha uangalizi na asionyeshe dalili.
WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**



## KINANA AMSAMEHE MCHUNGAJI MSIGWA

UKURASA 4

# Vigogo MSD kortini utakatishaji fedha

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO NAMUNGO FC YAJIPANGA KUZIBANA SIMBA, YANGA UK.23

MAONI, KATUNI UK.6



Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Laurean Rugambwa (kulia) na Mkurugenzi Mshauri Mkuu wa MSD, Byekwaso Tabura (wa pili kulia), wakiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijiji Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka matano ikiwamo kuratibu genge la uhalifu, kusababisha hasara na kutakatisha Sh. Bilioni 1.6. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JPM: HAKUNA CORONA

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli amesema kuwa Tanzania kwa sasa haina corona, hata hivyo amewataka wananchi kuchukua tahadhari, ikiwamo kuacha kuvaa barakoa za msaada na kuwataka kushona za kwao.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), jana jijini hapa, alisema kuwa hali ikiendelea hivyo, serikali inafikiria kuzifungua shule za sekondari, msingi na awali baada ya kukuridhika na mwenendo wa ugonjwa wa corona nchini.

"...Umekuja ugonjwa wa corona, walisema maiti zitazagaa hasa Afrika, walikuwa watabiri walishindwa kuelewa Mungu analipenda Taifa la Tanzania. Tuliomba siku tatu corona imekwisha...uzushi utatolewa wa kila aina tuwe makini," alisema.

Alisema: "Ugonjwa huu umepungua na nina uhakika utaisha kwa sababu Mungu yupo pamoja na sisi. Tulianza na Mungu na tutamaliza na Mungu."

Alisisitiza kuwa Tanzania imeshinda vita ya corona na itaendelea kushinda na ana uhakika hivi karibuni baada ya vyuo kufunguliwa wataangalia mambo yanavyokwenda ili kufungua shule za sekondari, msingi na hata za awali.

"Tunaangalia mambo yanavyoenda na shule za msingi na chekechea na hizi nazo zipo mbioni tutazifungua, ili walimu mkafanye kazi kwasababu nina fahamu walimu wa Tanzania wanapenda kufanya kazi,"alisema.

"Nimepata taarifa za Waziri wa Afya juzi, akisema Dar es Salaam kulikuwa na wagonjwa wanne, lakini uzushi utatolewa wa kila aina, Watanzania tumtangulize Mungu," alisema.

Alitoa wito kwa viongozi mbalimbali kutopokea vifaa vya corona ambavyo havijathibitishwa na Wizara na Afya.

"Kwasababu njia nyingine itakayotumika ni kuletewa vifaa vya corona vyenye corona, akikuletea mtu barakoa kataa, mwambie akavae yeye na mtoto wake na mke wake nyumbani, tutaumizwa, juzi nilikuwa nasikia kwenye taarifa ya habari kuna kundi songezi linajiita Magufuli 'forum' mimi hata silijui, sijui lakini sishangai mtu kujiita Magufuli, wanagawa barakoa sijui wametoa wapi," alisema.

Aliagiza viongozi wa wilaya na mikoa kukamata na kuhoji wanaogawa barakoa ili kujua zimethibitishwa na nani huku akitahadharisha watu kuwa wataumia kwa kukosa maarifa."Ukitaka kuvaa barakoa shona yako, kila Mtanzania achukue tahadhari, tusidanganywe kwa kuletewa barakoa ambayo hatujui yametoka wapi, tutaeneza corona bila sisi kujua, naamini ugonjwa huu utapungua kwasababu Mungu yupo pamoja nasi," alisema.

Aliwataka walimu wakatoe elimu hiyo kwa wananchi na kwamba tayari Tanzania imeshinda na ndege zimeanza kuja na kuwaomba watalii waendelee kuja nchini.

"Ndio maana sisi hatukuweka 'lockdown' (kujifungia) maana yake hakuna kitu ambacho kingefanyika, ukiji-lockdown umejiua huwezi kufanya kitu, waliendа mbali tulockdown makanisa na misikiti, wamesahau wakati wa shida watu walimkimbilia Mungu sisi tunakimbilia ndani, tulitaka kumpa utawala shetani badala ya Mungu," alisema.

Kadhalika, Rais Magufuli alisema kutokana na kazi kubwa inayofanywa na walimu, ndio maana hakuweza kusitisha mishahara ya walimu kipindi hichi cha ugonjwa wa corona.

Alisema ni vyema wananchi wakatambua kuwa kuna vita ya kiuchumi na hasa unapojenga uchumi wa kujitegemea.

"Tuliendelea kuwalipa walimu, Sh. bilioni 300 zinatumika kulipa mishahara ya walimu, serikali inatambua kazi mnayoifanya, niwahakikishie hata kama shule zingefungwa mwaka mzima au miaka 10 tungeendelea kulipa mishahara yenu kwasababu corona haikuletwa na walimu,"alisema.

### Amzungumzia Dk. Mwele

Alisema alipoingia madarakani ilitangazwa Tanzania kuna ugonjwa wa Zika na aliyetangaza na aliyetumiwa kutangaza alimfukuza kazi (Dk. Mwele Malecela).

"Baada ya kumfukuza kazi siku chache akateuliwa na wale waliomtuma kutangaza, baada ya miaka mitano hatujawahi kuwa na kesi ya Zika Tanzania, baadaye ilizuka tena ebola, tukasema sisi hatuna ebola..., waling'ang'ana wee sisi tukasema we have no ebola."

### Mwarobaini malipo hewa

Alisema ili kudhibiti malipo hewa, serikali inaandaa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya na kuhakiki madeni ya watumishi wa umma ikiwamo walimu.

Alisema mfumo utaanza kutumika kwa majaribio mwezi huu na utaanzia Mkoa wa Dodoma na itakapoonekana inafaa utatumika nchi nzima.

Alifafanua kuwa malimbikizo ya madeni ya mishahara na isiyo ya mishahara tangu Novemba 2015 imelipa Sh. bilioni 115.3, kati ya hizo Sh. bilioni 38.3, wamelipwa walimu 35,805 kwa mujibu wa taarifa juzi ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Alisisitiza kuwa kabla ya mwezi Agosti, mwaka huu, watakuwa wamelipa madeni ya walimu 2,631 waliobaki wanaodai kiasi cha Sh. bilioni 215.

### Afagilia uongozi CWT

Aliusifu uongozi wa CWT unaomaliza muda wake kwa kuwa umejenga ushirikiano wa dhati na serikali.

"Uongozi huu umejenga uhusiano mzuri na serikali na hata zilipojitokeza changamoto walikuwa wepesi kujadiliana na serikali kwa lengo la kutafuta ufumbuzi na ndio sababu hamkusikia msuguano na chama kama ilivyokuwa zamani,"alisema.

### Upandishaji vyeo

Alisema baada ya uhakiki watumishi 306,917 walipandishwa vyeo kati yao walimu 160,367 na mwaka huu wa fedha 2020/21, wanatarajia kupandisha watumishi 290,625 kati yao walimu ni 166,548.

Ajira mpya

Kwa miaka mitano serikali imeajiri walimu 22,341 na mwaka wa fedha unaoisha (2019/20) walimu 13,526 wataajiriwa wapya.

### Uchaguzi CWT

Kuhusu uchaguzi, Rais Magufuli alisema chama hicho ni taasisi muhimu sana kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya walimu.

Alisema viongozi watakaochaguliwa watambue wajibu wao ni kuwatumikia wanachama na sio kujinufaisha, wahakikishe mali zinatumika kwa malengo ya chama.

Aliwahimiza viongozi waendelee kututaua upungufu uliopo kwenye benki ya walimu ili wanachama wanufaike na matunda ya kuanzishwa kwake.

### Siku ya Mazingira

Rais Magufuli aliagiza Watanzania kupanda miti kwenye maeneo yao na walimu wawahimize wanafunzi kupanda miti hasa ya matunda ili kutunza maeneo.

Awali, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif aliomba walimu walioajiriwa mwaka 2013/14 wapandishwe vyeo katika bajeti ya 2020.

## Vigogo MSD washtakiwa kwa utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wawili wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani, Laurean Bwanakunu na mwenzake wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka matano.

Mashtaka hayo ni kuratibu genge la uhalifu, kusababisha hasara na kutakatisha Sh. bilioni 1.6 na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni tatu.

Kadhalika, Bwanakunu anakabiliwa na shtaka la kutoa nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa MDS bila kibali cha Katibu Mkuu wa Utumishi.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabati.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Faraja Ngukah, akisaidiana na waendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Fatuma Waziri na Sofia Nyanda.

Ngukah alimtaja mshtakiwa mwingine kuwa ni, Kaimu Mkurugenzi wa Logistiki wa MSD, Byekwaso Tabura.

Katika shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa, kati ya Julai mosi, 2016 na Juni 30, 2019, mahali tofauti jijini Dar es Salaam na nchini wakiwa watumishi wa umma waliratibu genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Upande wa Jamhuri ulidai shtaka la pili, kati ya Julai mosi, 2016 na Juni 30,2019 katika ofisi za MSD zilizopo Keko, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam washtakiwa kwa pamoja waliisababishia MSD hasara ya Sh. 3, 816,727,112.75.

Ngukah alidai katika shtaka la tatu, kati ya Julai mosi, 2016 na Juni 30, 2019 ofisi za MDS, Bwanakunu alitumia madaraka yake vibaya kwa kuidhinisha nyongeza ya mishahara Sh. bilioni 3.8 kwa watumishi wa MSD bila kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi.

Katika shtaka la nne, tarehe za tukio katika ofisi hizo, washtakiwa wote wawili wanadaiwa kushindwa kuhifadhi dawa na vifaa tiba, kitendo ambacho vilikosa ubora na kusababishia MDS hasara ya Sh. 85,199,879.65.

Shtaka la tano, tarehe za tukio katika ofisi hizo, washtakiwa walitakatisha Sh. 1,603,991,095.37 wakati wakijua ni zao la genge la uhalifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Ngukah alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuiomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Mawakili Peter Kibatala, Kenedy Mgongolwa, Oscar Magotosa na Khalaghe Hashim, ulidai hauna pingamizi.

Hakimu Kabate alisema washtakiwa wapelekwe rumande kesi itatajwa Juni 19, mwaka huu.

## HABARI KITAIFA

# Bunge labaini dosari sheria iliyolazimisha kumiliki laini 1

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

BUNGE limebaini dosari katika utungaji wa sheria ndogo nchini, ikiwamo sheria inayoweka zuio kwa mwananchi kuwa na laini ya simu zaidi ya moja.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana, taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika mikutano ya 18 na 19 ya Bunge, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, William Ngeleja, alisema miongoni mwa dosari hizo ni sheria ndogo kwenda kinyume cha sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Alizitaja baadhi ya sheria hizo kuwa ni pamoja na The Water Supply, Regulations 2019 ambayo inakwenda kinyume cha Sheria ya The Water Supply and Sanitation, 2019 na Sheria Ndogo (Ada na Ushuru) za Halmashauri za Mkinga 2019 inayokwenda kinyume cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290.

Ngeleja alisema dosari ya pili ni sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria, akiwakumbusha waandishi wa sheria kuzingatia kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachowataka kuzingatia majedwali kuwa sehemu ya sheria.

Mbunge huyo wa Sengerema (CCM) aliitaja dosari ya tatu kuwa ni sheria ndogo kuwa na makosa katika majedwali kwa kurejea kanuni ambazo si sahihi au kurejea kanuni ambazo hazipo.

Alisema dosari ya nne ni sheria ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ukiwamo urahisi katika utekelezwji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.

Alisema Sheria ya The Electronic and Postal Communication, Regulations 2020, imeweka masharti yasiyo na uhalisia yenye zuio la mtu kumiliki zaidi ya laini moja ya simu kutoka kampuni moja ya simu.

Vilevile, alisema wamebaini sheria ndogo kukiuka haki za binadamu, akiitolea mfano Sheria ya The Transport Licensing Act (Sura 317) ambayo mtu anaweza kufutiwa leseni bila hata kupewa nafasi ya kusikilizwa.

Alisema kuwa katika mikutano hiyo miwili, kamati yao ilipitia na kuchambua sheria ndogo 2,601.



Mafundi wa kampuni ya ukandarasi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ya mabasi ya mwendokasi, katika eneo la Mbagala Kizuiani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Takukuru yarejesha mil. 241/- Afya Saccos

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoa wa Temeke, jijini Dar es Salaam, imekabidhi Sh. milioni 241.303 kwa uongozi mpya wa Saccos ya Afya na kati ya hizo Sh. milioni 35.285 zimekabidhiwa kwa wastaafu 10, waliokuwa wanachama.

Fedha hizo zilizokolewa na Takukuru kutoka mkononi mwa aliyekuwa Meneja wa Afya-Temeke Saccos, Dunstan Kabelwa na aliyekuwa Karani wa fedha, Vailet Chengula, ambazo zilikuwa zikifanyiwa uchunguzi baada ya kubainika kuwapo kwa upotevu.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari juzi na Mkuu wa Takukuru mkoa wa Temeke, Donasian Kessy, ilieleza kuwa, Juni 7, mwaka 2018, ofisi yake ilipokea malalamiko yanayohusu ubadhirifu wa fedha za michango ya wanachama.

Alieleza zaidi kuwa, uchunguzi wa tuhuma hizo ulianza na kubaini ubadhirifu uliofanywa na majina ya watuhumiwa na baada ya mahojiano watuhumiwa walikubali kurudisha fedha hizo.

"Leo (juzi) Takukuru inayofuraha kukabidhi kiasi hiki cha fedha kwa uongozi mpya wa Afya Saccos. Kati ya fedha hizo Sh. milioni 35.285 tunazikabidhi kwa wastaafu 10 walikuwa wanachama wa saccos hii," alisema Kessy.

Alisema fedha zilizobakia zitaingizwa kwenye akaunti ya chama kwa ajili ya kuendelea na malipo kwa wanachama wengine waliokuwa wanadai.

Vile vile, alitoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwa namba ya bure 113 au kufika ofisi za Takukuru.

**"Leo (juzi) Takukuru inayofuraha kukabidhi kiasi hiki cha fedha kwa uongozi mpya wa Afya Saccos. Kati ya fedha hizo Sh. milioni 35.285 tunazikabidhi kwa wastaafu 10 walikuwa wanachama wa saccos hii," alisema Kessy**

# Aliyejifanya ofisa Takukuru matatani

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Kigoma, inamshikilia mkazi wa Kilimahewa Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Jafeti Emmanueli, kwa tuhuma za kujifanya ofisa wa Takukuru na kujipatia Sh. 90,000 kwa njia ya udanganyifu.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Nestory Gatahwa, alisema uchunguzi wa Taasisi hiyo umebaini kwamba, mtuhumiwa katika nyakati tofauti Mei, mwaka huu, amekuwa akijitambulisha kuwa ni ofisa wa Takukuru wa mkoa huo, kitengo cha sheria na pia kitengo cha kushughulikia migogoro mikubwa ya ardhi.

Gatahwa alisema utambulisho wake huo uliambatana na kuomba fedha ili aweze kutekeleza majukumu yake ya kikazi kama ofisa wa Taasisi hiyo.

Miongoni mwa maeneo ambayo alifika na kujitambulisha kwa cheo hicho ni ofisi za watendaji wa kata za Bangwe, Businde, Kagera, Mahakama ya Mwanzo Ujiji na Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Alisema katika kufanikisha nia yake ovu, mtuhumiwa huyo alijipatia Sh. 90,000 kutoka kwa mwananchi (jina linahifadhiwa) ikiwa ni sehemu ya Sh. 300,000 alizotaka kwa ajili ya kuwezesha kutenguliwa kwa uamuzi wa mahakama katika shauri la mgogoro wa shamba alilokuwa nalo.

Pia, alisema mtuhumiwa aliomba Sh. 500,000 kutoka kwa mwananchi mwingine ili amsaidie kupata kazi Takukuru, hata hivyo mwananchi huyo hakuwa tayari kutoa fedha hizo.

Alisema uchunguzi wa tuhuma hizo unaendelea na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani utakapokamilika.

Pia, Takukuru Mei 28, mwaka huu, Mahakama ya Wilaya ya Kasulu mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo Cresensia Mushi, ilimtia hatiani mshtakiwa Tilumanywa George Muzuma, aliyekuwa Mhasibu Msaidizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Mkoa wa Kigoma.

Alisema mshtakiwa huyo alifunguliwa shauri la jinai na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru Mkoa wa Kigoma Boniface Kamwesigile, Februari 25, 2019 katika Mahakama ya Wilaya ya Kasulu.

Alisema mshtakiwa huyo alishtakiwa kwa makosa ya kutumia nyaraka zenye maelezo ya uongo kumdanganya mwajiri, hivyo kumwezesha kujipatia Sh. 11,754,000.

Mwisho


## TAARIFA KWA UMMA

### TANGAZO LA NOTISI YA KULIPA DENI

Kwa idhini tuliopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LIMITED, CHAMPION AUCTION MART** tunatoa taarifa kwa wadaiwa wote kulipa deni unalodaiwa ndani ya Siku Kumi na Nne (14) ya tangazo hili baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako kwa majina yafuatayo kwenye jedwali hapo chini.

| MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| Mussa James Kazungu | Nyumba | Chanika Kwa Zoo- Mgeule | 22/06/2020 |
| Mangaza Khasim Said | Nyumba | Kimara-Mtaa Wa Temboni | 19/06/2020 |
| Nisile Boazi Mwakajumba | Nyumba | Majohe - Kichangani | 23/06/2020 |
| James Paul Kitonga | Nyumba | Kivule- Mbondole | 24/06/2020 |

**MASHARTI YA KUTOLIPA MADENI**

1. Atakayeshindwa kulipa deni lake analodaiwa kwa muda uliopangwa ndani ya siku kumi na nne baada ya tangazo kutolewa hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa.

215765002

**MAWASILIANO: CHAMPION AUCTION MART: 0653005019 /0756761328 /0687891122**

HABARI KITAIFA

# Kinana amsamehe Msigwa, kufundisha uongozi vyuoni

**Na Asraj Mvungi, ARUSHA**

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahaman Kinana, amempa 'toba' Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Mch. Peter Msigwa, ambaye aliomba amsamehe hadharani kutokana na kauli za uongo alizowahi kuzitoa dhidi yake.

Jana, Kinana akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, alisema ameamua kumsamehe Msigwa anayetoka chama kikuu cha upinzani nchini, kumfuata na kumuomba kiungwana kumsamehe kwa aliyoyasema dhidi yake kwa nyakati tofauti.

Kuhusu tuhuma alizitoa mbunge huyo kwamba kiongozi huyo wa zamani wa CCM, alikuwa anafanya biashara haramu za nyara za serikali, Kinana alisema: "Tuhuma za Mchungaji Msigwa zilikuwa nzito, na nilimpeleka mahakamani ambako hata hivyo alishindwa kuthibitisha na mahakama ikamtaka anilipe fidia."

"Baada ya kesi hiyo kusikilizwa mara 84, kwa muda wa miaka minne, Mchungaji alinitafuta kupitia kwa marafiki zake na kuniomba radhi, na baadaye tulikutana na nikaamua kumsamehe."

Mei 19, mwaka huu, akizungumza jijini Dar es Salaam, Msigwa alisema tuhuma zote alizowahi kuzitoa dhidi ya Kinana bungeni na kwenye mikutano ya siasa nje ya Bunge, hazikuwa na ukweli wala ushahidi wowote.

Msigwa alieleza: "Nidhahiri kwamba nimemkosea, nimemdhalilisha na kumkashifu ndugu yangu Abdulrahaman Kinana. Nimekutana na kuzungumza naye kuhusu jambo hili na kumuomba radhi. Ninashukuru kwamba amekubali kunisamehe."

"Bila shaka mtakubaliana nami kwamba Kinana ni mzalendo, muungwana na mstaarabu ambaye kwa kweli hastahili kukashifiwa wala kudhalilishwa. Nitaendelea kumheshimu kama alivyodhihirisha ustahimilivu na uungwana wake kwangu, kwa familia yangu na kwa Watanzania."

KUFUNDISHA UONGOZI

Alipoulizwa na Nipashe kuwa anatarajia kufanya nini baada ya kustaafu siasa, alisema anatamani sasa mambo yote aliyojifunza katika maisha yake ya uongozi serikalini na ndani ya chama hicho ayarithishe kwa vijana.

"Katika maisha yangu ya uongozi na hasa maisha yangu ya utendaji serikalini na ndani ya chama, nimejifunza mengi na nimekutana na mambo mengi, nimepata fursa ya kujifunza mambo mengi nimekutana na mambo mengi na pia nimeweza kuwa mwanafunzi wa vitendo."

"Ningependa yote hayo ambayo nimeyapata niwarithishe kwa wale ambao wanajiandaa kuwa viongozi katika siku za karibuni na siku zijazo. Mambo mengi nimejifunza hayapo kwenye vitabu, bali yanapatikana kwenye utendaji."

"Kila unapozunguka unaona mengi na unajifunza mengi, kwa hiyo ninatarajia kuendelea kutoa mchango wangu katika uzoefu wangu kwenye uongozi, ninatarajia na tayari nimepeleka maombi kwenye vyuo mbalimbali, na baadhi ya vyuo vimekubali nitoe mafunzo hasa katika masuala ya uongozi."

Alisema uongozi una mambo mengi likiwamo suala la uvumilivu na kuwa karibu na watu, kuwa mkweli, msiri na pia umuhimu wa kusoma, tena kusoma sana.

Mwisho

## Kortini akishtakiwa kukwepa kodi bil. 3/-

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Poison Batisha (36), amefikishwa mahakamani, akikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kukwepa kodi ya zaidi ya Sh.bilioni tatu, kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mfanyabiashara huyo alisomewa mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega.

Wakili wa Serikali Janeth Magoho, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Januari mosi, 2012 na Mei 12, mwaka huu, wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikwepa kulipa kodi kupitia bidhaa zake za kielektroniki zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Katika shtaka la pili, inadaiwa siku ya tukio mshtakiwa huyo aliisababishia hasara TRA ya fedha hizo, baada ya kukwepa kulipa kodi.

Katika shitaka la tatu, mshtakiwa anadaiwa kutakatisha Sh. 3,010,092,416 wakati akijua ni zao la kukwepa kodi.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya Uhujumu Uchumi.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Juni 18, mwaka huu na mshtakiwa alirudishwa rumande.

**Wakili wa Serikali Janeth Magoho, alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Januari mosi, 2012 na Mei 12, mwaka huu, wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikwepa kulipa kodi kupitia bidhaa zake za kielektroniki zaidi ya Sh. bilioni tatu.**



Makamu Mkuu wa chuo Kikuu cha Mt. Augustine Mwanza, Prof. Costa Mahalu (kushoto), akizungumza wakati wa mkutano na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Abdul-Razaq Badru (wa pili kulia), uliofanyika chuoni hapo, jijini Mwanza juzi. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Wanafunzi vyuo vikuu walipwa fedha kujikimu

**Na Mary Geofrey**

AGIZO la Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kutaka wanafunzi wa elimu ya juu kulipwa fedha zao za kujikimu ndani ya saa 48, limetekelezwa.

Juzi, Prof. Ndalicho alisema endapo vyuo vitashindwa kutekeleza agizo hilo, vitachukuliwa hatua za kisheria.

Nipashe jana lilizungumza na uongozi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Cha Tumaini, Dar es Salaam (Tudarco), ambao walithibitisha wanafunzi kuanza kulipwa na wengine kuendelea kulipwa.

Naibu Waziri wa Elimu wa Serikali ya wanafunzi wa Turdaco, Charles Magere, aliambia Nipashe kuwa, tayari wanafunzi walishaanza kuingiziwa fedha zao za kujikimu na wanaendelea kufanya hivyo kwa wanafunzi ambao bado hawajakamilisha taratibu.

"Tayari wanafunzi wameshaanza kulipwa kabla hatujafungua vyuo na wanaendelea kufanya malipo kwa wanafunzi isipokuwa kwa wachache ambao nao bado wapo kwenye 'process' (utaratibu) wa malipo," alisema Magere.

Mmoja wa wanafunzi wa Tudarco, Rose Mwijako, alisema, waliona tangazo la kuwasihi wanafunzi kwenda kuchukua malipo yao kwa ambao hawajafanya hivyo.

"Wanaendelea kulipwa na wengine wanalipwa na jana (juzi) nimeona tangazo wanasema wale ambao hawajaenda kuchukua fedha zao wafanye hivyo," alisema Mwijako.

Naye, Mwenyekiti wa Serikali ya Wanafunzi Daruso- SJMC, Swalehe Makoye, alithibitisha kuwa wanafunzi hao walianza kulipwa tangu Jumatatu, wiki hii.

Alisema kazi ya kuwalipa wanafunzi inaendelea na ambao hawajalipwa ni wachache wenye kasoro zinazofanyiwa kazi ili kukamilishiwa malipo yao.

Naye, Mwanafunzi wa UDSM, Joyce Mchome, alisema wanafunzi walishaanza kulipwa fedha zao na wengine wanaendelea kusubiria foleni yao kwa ajili ya kukamilishiwa.

Prof. Ndalichako alisema ni muhimu kwa agizo hilo kutekelezwa kwa wakati bila ya kuwapo kwa visingizio kutoka katika vyuo hivyo kwa kuwa tayari wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ilishajihakikishia kuwa mipango ya utoaji wa fedha hizo upo tayari na kilichokuwa kikisubiriwa ni mchakato wa vyuo hivyo pamoja na wanafunzi kurejea vyuoni.

HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi adaiwa kujiua kwa kujitumbukiza tangi la maji

**Na Rose Jacob, MWANZA**

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza, Fatuma Makaranga (15), amefariki dunia kwa madai ya kujitumbukiza ndani ya tangi la maji baada ya kutokea mtafaruku baina yake na familia yake.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Murilo Jumanne, alisema Juni 4, mwaka huu, majira ya saa 5.51 usiku katika mtaa wa Ndofe, wilayani Nyamagana, walipata taarifa za kifo hicho.

"Mwanafunzi aliyefariki anafahamika kwa jina la Fatuma Makalanga mwenye umri wa miaka 15 wa kidato cha kwanza katika sekondari ya Morning Star, alikutwa akiwa amefariki na mwili wake ukiwa ndani ya tangi la maji lililopo nyumbani kwao baada ya harufu mbaya iliyokuwa kitokea ndani ya tangi hilo," alisema Murilo.

Murilo alisema kifo hicho kimetokana na mtafaruku mkubwa uliotokea baina yake na baba yake mzazi na mwanafunzi huyo kuamua kuondoka kwao na kuelekea kusikojulikana.

"Baada ya wazazi wake kumtafuta bila mafanikio, walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi Nyakato na baada ya siku kadhaa kupita walianza kusikia harufu mbaya ikitokea ndani ya tangi hilo, ndipo baba alipoamuru wamwage maji walifanyie usafi. Shughuli ya kusafisha ilianza ndipo walipokuta mwili wa binti huyo," alisema Murilo.

Alisema uchunguzi wa tukio hilo unafanywa ili kubaini chanzo chake.




Kamanda wa Polisi mkoa wa Mwanza, Murilo Jumanne (katikati), akikabidhi sehemu ya vifaa vya ofisini zikiwamo kompyuta na printa kwa Kamanda Msaidizi wa mkoa huo, Saphia Jongo, vilivyotolewa msaada na wadau wa maendeleo wa KAT Computer na wengine, kwa ajili ya matumizi ya jeshi hilo, jijini Mwanza jana. **PICHA: ROSE JACOB**

# Jafo awacharukia watumishi kufanyakazi kimazoea

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ,Selemani Jafo, amewataka watumishi wa umma kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alisema hayo wakati akizungumza na Wakuu wa wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri mkoani Kagera, kuhusu mienendo ya miradi ya maendeleo mkoani hapo.

Waziri Jafo alisema Halmashauri ya Wilaya Biharamulo, haina historia nzuri ya ukusanyaji wa mapato na kutakiwa kupambana kadiri inavyoweza ili kuwa na mapato yanayoridhisha.

"Halmashauri hii haina historia nzuri sana katika shughuli ya ukusanyaji mapato kwa kupindi kirefu, hivyo lazima mkurugenzi kupambana kadiri anavyoweza katika suala la mapato," alisema Jafo.

Alisema uendeshaji wowote unahitaji ukusanyaji wa pato ili wizara isiweze kuyumba katika kutatua matatizo ya wananchi.

Jafo alisema, makusanyo hayo huelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, miundombinu ya barabara na maji.

Alisema kwa mkoa huo kuna ujenzi wa hospitali tatu za Wilaya ya Kyerwa inayogarimu Sh. bilioni1.5, Karagwe Sh. bilioni 1.5 na Bukoba, Sh. bilioni 1.5.

Kadhalika, alisema hospitali hizo zinatakiwa kufikia Juni 8, zianze kutoa huduma kwa wananchi na kutovuka muda uliopangwa.

Alisema usimamizi wa miundombinu ya barabara unaofanywa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), ukakikishe unafuata muda licha ya kuwa na changamoto ya ucheleweshaji kwa baadhi ya barabara.

Alisema miradi yote iliyo chini ya Tamisemi utendaji wake ufuate taratibu zinazotakiwa na unaoridhisha na kuacha mazoea.

Pia, alisema Rais John Magufuli, alitoa Sh. bilioni 800 kwa nchi ziweze kutekeleza miundombinu ya barabara miji minane kwa kiwango cha lami.

# Mbaroni wakituhumiwa kumiliki silaha kinyume

**Na Welingtone Masele, TABORA**

JESHI la Polisi mkoani hapa limewakamata watu watatu kwa tuhuma za kumiliki bunduki tano kinyume cha sheria.

Akitoa taarifa mbele ya waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, ACP Barnabas Mwakalukwa, alisema Mei 29, mwaka huu, askari walimkamata Said Ramadhan (35), mkazi wa Ipuli Kidatu B, ambaye alikuwa akijihusisha na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kukutwa na silaha tatu ambazo ni shotgun, magobore mawili, risasi moja ya shotgun, maganda matatu ya risasi za shotgun pamoja na baruti.

Katika tukio jingine, Mei 29 katika kijiji cha Usinge, wilayani Kaliua, polisi ilimkamata Dotto Hamis (22), akiwa na silaha aina ya shotgun iliyotengenezwa kienyeji ikiwa na risasi moja ya shotgun, kwenye silaha hiyo ambayo huitumia kufanya uhalifu.

Pia, Machi 30 katika kijiji cha Imalampaka, wilayani Kaliua, polisi ilimkamata Nyengi Dotto (37), akiwa na silaha moja aina ya gobole iliyotengenezwa kienyeji akiwa ameificha kwenye majani ya ua wa choo.

Kamanda Mwakalukwa alisema kutokana na ushirikishwaji wa jamii na elimu inayotolewa kwa wananchi, imesaidia wananchi hao kusalimisha silaha tatu aina ya gobole ambazo zilikuwa zinamilikiwa kinyume cha sheria.

Misako mbalimbali inayoendelea katika maeneo Tabora, ilimefanikisha kumkamata Halfani Omari na wenzake wanne wakiwa na gunia la bangi ambalo waliligawa katika viroba vitano vya mahindi kwa lengo la kuiaminisha jamii kuwa anasafirisha mahindi kwenda mkoa wa Dar es Salaam.

Kamanda Mwakalukwa alisema jeshi hilo linawashikilia pia watuhumiwa tisa wanaojihusisha na matukio ya mauaji ya askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), tukio lililotokea maeneo ya Ipuli, Mei 30, huku watuhumiwa wengine wakiendelea kusakwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Makocha, washambuliaji wazawa amkeni Ligi Kuu

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Juni 13, mwaka huu baada ya kusimama kwa muda wa zaidi ya miezi miwili ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), ambao umeitingisha dunia.

Tayari Shirikisho la Soka Nchini (TFF), limeshatangaza ratiba ya mechi za ligi hiyo ya juu kwa upande wa Tanzania Bara ambayo ilikuwa inaelekea ukingoni.

Ligi hiyo ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati mashindano ya Kombe la FA ambayo nayo yataendelea kuanzia mwisho wa mwezi, hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hadi ligi hiyo inasimama, mabingwa watetezi, Simba ndio walikuwa wanaongoza katika msimamo wakiwa na pointi 71, baada ya kushuka uwanjani katika michezo 28, ikibakiwa na mechi 10 ili kumaliza msimu.

Nafasi ya pili katika msimamo inashikiliwa na Azam FC yenye pointi 54 huku Yanga yenye mchezo mmoja mkononi ikifuatia baada ya kujikusanyia pointi 51 kibindoni.

Kwa maana hiyo, Simba inayonolewa na Kocha Mbelgiji Sven Vandenbroeck imempita Azam FC pointi 17 huku ikiwaacha watani zao, Yanga kwa tofauti ya pointi 20, lakini timu hizo zote tatu zinafundishwa na makocha kutoka mataifa mengine.

Azam yenyewe inanolewa na Aristica Cioaba ambaye ni raia wa Romania wakati Yanga iko chini ya Mbelgiji Luc Eymael.

Nipashe inawakumbusha na kuwaamsha makocha wazalendo kujipanga upya na kuandaa mipango ya kuhakikisha msimu ujao wanafanya vema na kuwa kwenye mbio za ubingwa kama ilivyo kwa wageni hawa.

Hakuna jambo linaloshindikana kwa sababu wachezaji wengi wanaowasaidia makocha hawa wa kigeni kupata matokeo mazuri, wamekulia kwenye mikono ya walimu wazalendo, lakini inapofika kwenye mbio za kuwania ubingwa, hawaonekani.

Katika mbinu zile zile zilizotumika kukuza vipaji hivi na baadaye wachezaji hao kusajiliwa na vigogo hao wa jijini Dar es Salaam, zinatakiwa kuendelea kuonekana katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Bara huko waliko.

Kama iliwezekana kwa klabu ya Leicester City kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City, Manchester United, Liverpool, au Chelsea, vile vile inawezekana kwa Kagera Sugar, Coastal Union au Polisi Tanzania, zinazofundishwa na makocha wa hapa nchini kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Nipashe linawataka makocha hao kuwaandaa wachezaji wao kwa kuwaambia wanaweza na kusahau kuhusu changamoto walizonazo, kwa sababu hakuna timu ambayo inapata huduma zote kwa asilimia 100.

Endapo Simba itafanikiwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, inamaanisha kwa msimu wa tatu mfululizo, hakuna kocha mzalendo ambaye ameweza kutwaa taji hilo lenye heshima nchini kwa upande wa soka.


Pia lipo suala la mbio za kuwania kiatu cha dhahabu, licha ya kuwa lolote linaweza kutokea kwenye mchuano huo.

Hadi mechi za Ligi Kuu Bara zinasimama, mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere ndiye alikuwa anaongoza, baada ya kuzifumania nyavu mara 19, akifuatiwa na Paul Nonga wa Lipuli, Reliants Lusajo (Namungo) na Yusuph Mhilu wa Kagera Sugar ambao kila mmoja ana mabao 11.

Washambuliaji wa zawa mnatakiwa kujiuliza mlipokosea ili ikiwezekana katika michezo iliyosalia mfanye vema zaidi na kumweka kwenye ushindani Kagere ambaye kama atakuchukua tuzo hiyo tena mwaka huu, itakuwa ni ya pili mfululizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Yanga yaingia kwenye mtihani

Na Barnabas Maro

'MTIHANI' ni utaratibu wa kupima maarifa aliyonayo mwanafunzi kuhusu somo alilofunzwa. Msukosuko unaomfika mja katika maisha; majaribu.

Maswali yanayojibiwa chini ya usimamizi maalumu ili kupima maarifa aliyonayo mtu anayepimwa. Tatizo ambalo Mungu humzushia mtu ili kumjaribu imani yake.

Kabla ya uongozi wa sasa wa Yanga kuingia madarakani, klabu hiyo ilikuwa ikiendeshwa vizuri bila matatizo. Baada ya kuondoka ndipo wanachama na wasio wanachama wakabaini umuhimu wao. Klabu iliyumba mpaka ikaitwa 'watembeza bakuli,' yaani kuomba fedha ili kuisaidia.

Ni dhahiri kuwa wapo watu na kampuni (sio 'makampuni' ) kadhaa zilizokuwa na nia ya kuisaidia Yanga lakini kutokana na viongozi kutokuwa na maono ya muda mrefu wakakata tamaa, hivyo klabu iliyumba sana.

Yanga ilikuwa na wakati mgumu kusajili wachezaji wa maana kwa kutokuwa na fedha. Hata kulipa mishahara ya waliokuwapo ilikuwa shida na baadhi yao kudai fedha zao za usajili!

Ilivyokuwa wakati ule, Yanga ilikuwa ikishinda kwa kubahatisha katika michezo yake. Hali hiyo iliwakatisha tamaa, si wanachama na wapenzi wake tu bali pia wachezaji waliokusudia kusajiliwa na timu hiyo. Mchezaji gani angejiunga na Yanga ilhali waliokuwapo hawakulipwa kwa miezi mitatu na kuendelea?

Kama hiyo haikutosha, baadhi yao na mashabiki wakaacha kwenda uwanjani kuishangilia. Wachache waliojinusuru kwenda uwanjani, hawakujaza eneo la Yanga. Hivyo eneo la Yanga likatwaliwa na idadi kubwa ya wapenzi wa Simba!

Jambo hili likaongeza pigo kwa Yanga ikilinganishwa na Simba iliyokamatwa barabara na kijana bilionea wao, Mohammed Dewji maarufu Mo.

Hii ilisababisha hata wapenzi na wanachama wa Simba waliokuwa wamekata tamaa kwenda uwanjani, wakarejea kila timu yao ilipokuwa na mechi. Wakajaza eneo kubwa la Yanga waliokuwa wamekata tamaa na timu yao!

Katika miaka ya '60 Yanga iliitwa 'foo-o-foo' kwani mara kwa mara ilipocheza, ilifungwa mabao manne! 'foo-o-foo' ni aina ya magari yaliyoitwa Peujeot 404.

Sitaki kueleza mengi ya wakati uliopita kuhusu Yanga, kwani hata Wahenga walisema: "Iliyopita si ndwele, tugange yajayo."

Maana yake ugonjwa uliokwishapita huwa si chochote hata kama ulikuwa mkali vipi; almuradi umeshapita haumshughulishi mtu kama unaokuja. Methali hii yatufunza umuhimu wa kujiandalia matatizo au shida zijazo badala ya kuziwazia zile zilizopita.

Sasa Yanga ina udhamini wa kampuni ya GSM inayoonekana kuwa na mipango mizuri kwa timu hiyo iitwayo ya 'wananchi.'

Kwa juhudi za GSM, sasa Yanga imewekeana mkataba na kampuni inayoendesha Ligi Kuu Hispania (La Liga) wa udhamini wake.

Endapo mpango huo utafanikiwa, basi Yanga itakuwa na uwezekano wa kupata mafunzo ya wachezaji, makocha na viongozi kutoka klabu ya Sevilla ya Hispania.

Vilevile Yanga itacheza mechi mbili moja Tanzania na nyingine Hispania kwa mwaka kati yake na timu maarufu ya Sevilla. Aidha kutakuwa na fursa ya wachezaji chipukizi wa Yanga kujiunga na shule ya michezo ya timu ya Sevilla yenye historia kubwa.

Wataalamu wa Sevilla watakuwa wakija Tanzania kutoa mafunzo ya uongozi kwa sababu mfumo utakaotumiwa na Yanga ni lazima uendane na ujuzi na uzoefu katika masuala ya uongozi, kwa mujibu wa mkataba uliotiwa saini majuzi.

Makubaliano ya mkataba huo ni kwamba huduma ya ushauri wa Yanga, La Liga na GSM utagharimu Sh. bilioni 2.6 kwa miaka mitatu.

GSM itagharimia shughuli zote za wataalamu wa La Liga watakaokuwa na ofisi yao kwenye jengo la kampuni hiyo barabara ya Samora jijini Dar es Salaam.

Wakati hali ikiwa hivyo, Rais wa klabu ya Sevilla, Jose Castro, Carmona alisema anafurahi Yanga kuwekeana mkataba na La Liga na Sevilla kwani anaridhishwa na ujuzi na uzoefu walionao katika masuala ya kandanda, uongozi na uwekezaji.

Naye Mkurugenzi wa biashara wa kimataifa wa La Liga, Juan Botella alisema amefurahi kuingia mkataba na Yanga inayokuwa klabu ya kwanza Afrika. Alisema kampuni yao yenye wataalamu wa kimataifa, watashirikiana na Sevilla kuhakikisha Yanga inakuwa na mfumo wa kisasa katika uendeshaji wa klabu.

Kwa upande mwingine, Mkurugenzi wa Kimataifa wa Masoko na Biashara wa Sevilla, Oscar Mayo alisema makubaliano yao na Yanga yanakusudia kuleta maendeleo ya ufundi, masoko na uongozi.

Sasa wanachama na mashabiki wa Yanga wanapaswa kuwa wamoja wakati klabu yao ikijengwa upya. Wasikubali kughilibiwa na baadhi ya viongozi wanaopinga mkataba huo kwa kukosa nafasi ya kuinyonya Yanga. Ikiwezekana wawaumbue hadharani ili watolewe kwenye uongozi. Salaam aleikum jamii.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 098**

# RC Mwanza akabidhi majina waliohusika upotevu mil. 274/-

**Na Neema Emmanuel, UKEREWE**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella amekabidhi majina ya watu watano wakusanya mapato wa halmashauri hiyo waliohusika na upotevu wa Sh. milioni 274.6 kwa Mkuu wa Polisi wilaya (OCD) na Mkuu wa Takukuru wa Wilaya ya Ukerewe.

Pia, wanadaiwa kupoteza mashine za kukusanyia mapato ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao ikiwamo kurejesha fedha.

Akizungumza katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mongella alisema serikali haitofumbia macho vitendo vya ubadhirifu wa fedha unaofanywa na mawakala kwa lengo la kujinufaisha.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Leopard Musiba, Fortunatus Mutesigwa, Thomas Bagetilanya, Frola Ntale na Didas Majura, na kutaka watafutwe popote walipo.

Alisema fedha hizo zilikusanywa, lakini hazikupelekwa benki na kutoa wiki moja kwa Takukuru na OCD kuhakikisha fedha hizo zinaingizwa kwenye akaunti ya halmashauri.

"Nataka niletewe stakabadhi za kuthibitisha kuwa fedha hizo zipo salama, pia mashine hizo zipatikane ili tuzipitishe kwenye mfumo tujue zimekusanya shilingi ngapi," alisema.

Kwa upande wao baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo, walisema mbali na upotevu wa fedha hizo bado kuna sintofahamu kuhusu stahiki zao ambazo zipo kisheria na mpaka sasa bado hawajalipwa ilhali Bunge linaelekea kuvunjwa.

"Tunaidai halmashauri fedha zetu za vikao kila tunapohitaji tulipwe tunalipwa nusu huku fedha zingine tunazungushwa, haijulikani tutalipwa lini," alisema diwani mmoja.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (wa tatu kushoto), akipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona kutoka kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Gasper Kileo, mjini Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Apinga magari yaliyokaa gereji miaka saba kuuzwa

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, amekataa mapendekezo ya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya mji Masasi ya kutaka kuuza magari matatu yaliyokaa gereji kwa miaka saba.

Pia, ameagiza magari hayo kufanyiwa matengenezo ndani ya miezi saba na kuendelea kutumiwa na halmashauri.

Byakanwa alitoa agizo hilo jana wilayani Masasi, wakati wa kikao malaamu cha Baraza la Madiwani lililoketi kwa ajili ya kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema kitendo cha madiwani hao kutoa hoja inayopendekeza kuuzwa kwa magari hayo kwa madai kuwa yameshindikana kutengenezwa kwa sababu halmashauri kukosa fedha za kuyatengeneza, hoja hiyo haina mashiko.

Byakanwa alisema halmashauri ina uhaba mkubwa wa magari ya kutolea huduma katika kutekeleza shughuli za halmashauri, hivyo kupitisha mapendekezo ya kutaka kuuza magari hayo, ambayo iwapo yatatengenezwa yatasaidia shughuli za halmashauri na uamuzi huo hauna busara.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona mali hiyo ya halmashauri inakaa kwa mzabuni kwa muda mrefu halafu halmashauri na madiwani wanashindwa kufanya uamuzi wenye afya na kuamua yauzwe bila kuangalia faida au hasara kwa halmashauri hiyo.

"Nakuomba Mkurugenzi tafuta fedha kokote unakojua zitengeneza haya magari, natoa miezi saba yawe tayari yametengenezwa haraka iwezekavyo mimi kama RC sioni sababu ya msingi ya ninyi madiwani kupendekeza kuuzwa," alisisitiza Byakanwa.

Mkuu huyo alisema menejimenti na baraza hilo inapaswa kujitathmini kwa kila uamuzi wanaofanya.

Akizungumzia kuhusu magari hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alisema magari kwa sasa yana zaidi ya miaka saba tangu yapelekwe kwenye matengenezo, lakini fedha za matengenezo yake hazijapatikana ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 30.

Alisema Baraza la Madiwani kupitia kamati ya mwaka 2017 ilipitisha mapendekezo ya kuitaka halmashauri itenge fedha hizo, lakini hazijapatikana na madiwani hao kuamua yauzwe ili fedha zitakazopatikana zitumike kwa shughuli zingine za maendeleo.

Naye, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Sospeter Nachunga, alisema madiwani wamepokea maagizo hayo na watahakikisha halmashauri hiyo inatafuta fedha hizo na kuyatengeneza magari.

# Halmashauri yatakiwa kuwajibisha watumishi kukosesha fedha miradi

**Na Gurian Adolf, NKASI**

SERIKALI mkoani Rukwa umeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani humo, kuwachukulia hatua kali za kinidhamu watumishi wanaosababisha kupata hati ya mashaka na kukosa fedha kwaajili ya miradi ya kimkakati.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, wakati akihutubia Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo ambalo limekutana kujibu hoja 84 kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambazo zimeongezeka kutoka hoja 32 mwaka 2018/2019 hadi kufikia hoja 84.

Wangabo alisema, akiwa msimamizi wa halmashauri zote mkoani humo, hayuko tayari kuona baadhi ya halmashauri zinakosa fedha za miradi kwasababu ya utendaji kazi mbovu wa watumishi na kutaka lazima wawajibishwe.

"Kumekuwa na uzembe kwa baadhi ya watumishi ambao wanasababisha kuongezeka kwa hoja na kutojibu kwa ufasaha hoja za CAG na hawa nina waona kama kikwazo cha maendeleo ya wananchi, miradi ya maendeleo ikikosekana wananchi nao hawapigi hatua, ni lazima wawajibishwe," alisema.

Aliwashauri baadhi ya wajumbe wa baraza waliokaa muda mrefu ambao ni madiwani, kutogombea katika uchaguzi mkuu ujao kwa kuwa ni wakati sasa wa kutoa nafasi kwa watu wengine hasa vijana ili wapeleke mawazo mapya.

Alisema ni vizuri wakastaafu kwa heshima wao wenyewe kuliko kusubiri kuanguka katika uchaguzi mkuu kwa sababu kutawasababishia aibu na sonona na matokea yake kuugua ugonjwa wa shinikizo la damu.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Zeno Sumuni, alisema kitendo cha baraza kukutana kujadili hoja hizo za CAG kina maanisha kuwa kuna watumishi ambao hawatimizi wajibu wao na kuibuka hoja hizo.

HABARI KITAIFA

# Mwanamke alalamika muuguzi kusababisha kifo cha mwanawe

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

MKAZI wa Kata ya Mhongolo Halmashuari ya Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga, Zahara Ismail (39), amemtuhumu nesi (jina limehifadhiwa) wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji huo kusababisha kifo cha mtoto wake kilichotokea Mei 10, mwaka huu, wakati akijifungua.

Hata hivyo, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. George Masasi, amekanusha madai hayo na kueleza kuwa chanzo cha kifo hicho ni mama kunywa dawa za kienyeji za kuharakisha uchungu ili ajifungue haraka.

Awali, mama huyo aliiomba serikali kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika chumba cha wajawazito ili kuokoa maisha ya mama na mtoto, huku akieleza kuna matumizi ya lugha mbaya na huduma hafifu.

Akisimulia yaliyomkuta alisema alipata usumbufu mkubwa wakati wa kujifungua na kwamba aliumwa uchungu na kwenda kuwaona manesi baada ya kuwaeleza hali yake walimpa kitanda, lakini baadaye alipopimwa na nesi aliambiwa njia haijafunguka na kutakiwa kurudi kusubiri licha ya uchungu mkali aliokuwa nao.

Alilalamika kuwa licha ya kuwa na maumivu makali na mtoto kuanza kushuka, nesi alimwambia arudi afanye mazoezi akiwa karibu na manesi ndipo aliporudi na kutandika mfuko chini na kulala na alipoanza kusukuma alimuita nesi huyo ambaye alidai alikataa kwa madai njia haijafunguka.

"Baada ya kulala chini kwenye sakafu nilimwita nesi nikamweleza nahisi kusukuma, lakini alinijibu 'wewe naye usitusumbue kwanza njia haijafunguka' na kudai 'wewe umelala hapo chini kwa jinsi tulivyochoka unategemea tukufuate hapo ili kukupima? Hakuna mtu mwenye mgongo wake kuja kuinama hapo kukupima'," alimnukuu nesi hiyo.

"Nilipokazana kusukuma nesi huyo simjui jina lake, alifika kunipima na kukuta njia imefunguka ndipo nikasukuma na mtoto akatoka na akaniwekea kifuani, nilivyomshika mwanangu alikuwa anapumua, hata hivyo sikuongea chochote. Nesi huyo alimuita mwenzake ambaye alikuja na mkasi na kukata kitovu kisha akamchukua mtoto," alisimulia mwanamke huyo.

Aliendelea kusimulia mkasa huo nesi alimkuchukua mtoto wake na kumpeleka sehemu ambayo hutunzwa watoto wanapozaliwa na aliporudi alimweleza amemuweka kwenye mpira wa oksijeni na kuonyeshwa mwanawe.

Alisema akiwa eneo la mapumziko alijulishwa mtoto wake amefariki na anaamini uzembe umechangia kifo cha mwanawe.

Baba wa mtoto aliyefariki, Ramadhani Bakari alisema amesikitishwa na tukio hilo kwa kuwa alishapokea taarifa za mkewe kujifungua salama na kwamba kama amefariki ni mpango wa Mungu.

Dk. Masasi alisema mama huyo alipokelewa hospitalini humo Mei 9, na alipata uchungu mkali huku njia ikiwa haijafunguka, na kwamba aliambiwa akae kitandani lakini alikataa.

Aidha, Dk. Masasi alikanusha madai kuwa mtoto huyo alifariki kukosa chakula, kwa kuwa kitaalam mtoto anaweza kukaa masaa 72 hajanyonya mara tu baada ya kuzaliwa.

Kwa mujibu wa Mganga huyo, vifo vya mama na mtoto vimepungua kutoka 24 hadi 8 kwa kipindi cha mwezi mmoja na kwa upande wa watoto wachanga vifo vimepungua kutoka 24 hadi 5 kwa mwezi.



Vijana wakipima vyuma chakavu kwaajili ya kuviuza kwa mnunuzi, katika eneo la Magole Chamazi, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Kutokana na kukosekana kwa ajira na kufanya hali ya maisha kuwa ngumu, vijana wengi wamekuwa wakijitafutia kipato kwa njia mbalimbali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kasesela apiga marufuku polisi kubambikia kesi wananchi

**Na francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, amepiga marufuku baadhi ya askari polisi wilayani hapo wanaodaiwa kuwabambikia wananchi kesi kwa sababu ya chuki binafsi zikiwamo za kunyimwa penzi au kulazimisha rushwa.

Alisema anapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaompigia simu na kufika ofisini kwake kulalamikia vitendo vya uonevu vinavyofanywa na baadhi ya askari polisi kwa kuwabambikizia kesi na kuwataka kutoa rushwa na kutaka likome mara moja .

Akizungumza na askari kata wa Wilaya ya Iringa, katika kikao chake cha kutatua changamoto za wananchi, Kasesela alisema, baadhi ya askari wanalichafua Jeshi la Polisi kutokana na tabia mbaya za kuonea raia.

"Wapo baadhi ya askari wa kike ambao wanawabambikizia kesi wanawake kutokana na wivu wa kimapenzi na wapo askari wa kiume ambao nao wanawabambikizia kesi wanaume wenzao baada ya kuzidiana kete kwa wanawake...niruhusuni siku moja nitoe mafunzo ya ziada jinsi ya kutongoza mademu wazuri na wanaume wazuri kuliko kuwabambikizia kesi kwa chuki binafsi," alisema.

Kasesela alisema, mmoja kati ya wenyeviti wa serikali katika wilaya hiyo amebambikiziwa kesi ya meno ya tembo kutokana na chuki binafsi jambo ambalo analiona linazidi kuota mizizi katika wilaya hiyo.

Alisema baada ya kuingia IGP Simon Sirro na kupiga marufuku mchezo wa askari kubambikizia watu kesi, alitegemea suala hilo lingekuwa ni historia, lakini anaendelea kukutana nalo.

Aliwataka askari kufanya kazi zao kwa weledi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu kwa kuwa ndio kipindi cha watu kubambikiziwa kesi zisizo na kichwa wala miguu kutokana na chuki binafsi ama kutumiwa na baadhi ya wanasiasa kufanya hivyo.

"Kipindi hiki ni kipindi kigumu, wananchi hawapaswi kunyanyasika, wakinyanyasika watashindwa kuichagua Serikali ya CCM na mimi kama DC nitaanza kulazimika kujieleza kwanini kura zimepungua, kumbe sababu kubwa ni manyanyaso ya polisi dhidi ya raia wasio na hatia," alisema.

Kasesela aliwataka polisi kuendelea kutunza siri za raia wanaofika vituoni kutoa taarifa mbalimbali ili kujenga imani kwa jeshi hilo.

Katika hatua nyingine Kasesela alipiga marufuku polisi kunyanyasa wafanyabiashara wa baa ambao wamezidisha muda wa kufunga badala yake wawazuie kupiga muziki nyakati za usiku na kama watajifungia ndani na kuendelea kunywa hakuna tatizo.

Hata hivyo, ameliruhusu jeshi hilo kuwamamata watakaokutwa wakinywa pombe asubuhi hata kama wauzaji wana vitambulisho vya ujasiriamali kwa kuwa hakuna sheria inayoruhusu watu kunywa pombe muda wa kazi.

## Vodacom yazindua Hadithi za Shigongo

**Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu za mkononi ya Vodacom Tanzania (PLC) kwa kushirikiana na Global Publishers, wamezindua huduma mpya ijulikanayo kama Hadithi za Shigongo ambayo itapatikana kwa watumiaji wa Vodacom pekee.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo juzi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Huduma za Kidijitali wa Vodacom, Nguvu Kamando, alisema kupitia huduma hiyo ya hadithi za Shigongo itasaidia kuburudisha na kuelimisha wateja wao.

Alisema wanaamini muungano huo kati ya Vodacom, Global Publishers na kampuni ya teknohama ya Premier Mobile Solutions, utaleta huduma bora kwa mteja wa Vodacom na wataanza na hadithi na simulizi mbalimbali na baadaye huduma nyingine za kuelimisha na kuburudisha jamii kwa jumla.

Alisema mteja wa Vodacom anaweza kujiunga kwa njia mbili, ya kwanza ni kwa kupiga namba 0901767676 na kufuata maelekezo au njia ya pili mteja anaweza kutuma neno Shigongo kwenda namba 15460. Akishajiunga atapokea ujumbe wa uthibitisho na kulipia Sh. 100 kwa huduma ya siku, Sh 450 kwa huduma ya wiki au Sh 1,000 kwa huduma ya mwezi na kisha kujulishwa jinsi ya kusikiliza hadithi yake.

Mkurugenzi wa Global na mtunzi mahiri wa riwaya, Eric Shigongo, alisema watu wengi wamekuwa na majukumu katika kujenga uchumi wa taifa hivyo kukosa muda wa kusoma vitabu.

"Kwa zaidi ya miaka 22 sasa nimekuwa nikiandika vitabu vingi na riwaya nyingi ambazo zimesomwa na Watanzania wengi. Kwa sababu watu wengi wana majukumu mengi, wanapenda kusoma riwaya zangu lakini wanakosa muda wa kukaa chini na kusoma.

"Kwa kushirikiana na Vodacom tunakujia na utaratibu mpya wa kurekodi vitabu vyote kwa mfumo wa sauti. Sasa utaweza kusikiliza hadithi ukiwa mahali popote kwa kutumia simu yako.

Alieleza kuwa kuwa kuanza watatoa hadithi ya kusisimua ya Damu na Machozi, ambayo inaeleza mapambano katika maisha, machozi na damu zinazomwagika wakati wa mapambano hayo mpaka mtu anapofikia mafanikio. Ni matumaini yangu kwamba utaburudika vya kutosha," alisema Shigongo.

# Katika kila Watanzania 10, mmoja anatumia tumbaku

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

IMEELEZWA kuwa, mtu mmoja kati ya 10 wenye umri wa miaka 15 au zaidi nchini, anatumia tumbaku.

Vilevile, wastani wa matumizi ya fedha kwa ajili ya tumbaku kwa mtu mmoja kwa mwezi, Sh. 28,840.

Hayo yalielezwa juzi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipokuwa akizindua ripoti ya utafiti wa matumizi ya tumbaku kwa watu wazima wa mwaka 2018 nchini.

Alisema wavutaji wa tumbaku wako hatarini kuyumba kiuchumi na kupata magonjwa yasiyoambukizwa kama tahadhari hazitachukuliwa mapema.

Waziri Ummy alisema kiwango hicho cha fedha wanachotumia, kingetosha kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi.

"Hii fedha ingetosha kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kwa mtu mmoja mmoja kwa mwezi kwa asilimia 58 na umaskini wa kupindukia (mahitaji ya chakula) kwa mtu mmoja mmoja kwa mwezi kwa asilimia 85," alisema.

Kiongozi huyo wa wizara alisema kwa kutumia taarifa za Matokeo ya Viashiria Muhimu vya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa Tanzania Bara wa Mwaka 2017-18, fedha za kujikimu kwa ajili ya mahitaji ya msingi kwa mwezi kwa mtu mmoja ni Sh. 49,320 na mahitaji ya chakula kwa mwezi kwa mtu mmoja ni Sh. 33,748.

Kwa mujibu wa utafiti huo, mtu mmoja kati ya 10 (8.7%) wenye umri wa miaka 15 au zaidi nchini, anatumia tumbaku ya aina yoyote na hivyo kuwa na watu milioni 2.6 kati ya watu zaidi ya milioni 55.

"Kati ya idadi hiyo, wanaume ni asilimia 14.6 na wanawake ni asilimia 3.2, pia watu nne kati ya 10 (40.3%) nchini wamewahi kuona onyo la matumizi ya tumbaku kupitia redio au runinga," alisema.

Waziri huyo alisema matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa, watu tisa kati ya 10 (92.3%) wenye umri wa miaka 15 au zaidi wanaamini uvutaji wa sigara husababisha magonjwa, wakati watu wanane kati ya 10 (84.4%) wanaamini kuvuta hewa ya mtu anayevuta sigara kunaweza kusababishia magonjwa hata kama wao hawavuti sigara.

"Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, taarifa inaonyesha kuwa watu wanne kati ya 10 (32.9%) wameathiriwa na moshi wa tumbaku sehemu za kazi ikiongozwa na sehemu za mabara na kumbi za starehe kwa asilimia 77 (watu milioni 3), maeneo ya huduma za biashara za vyakula asilimia 31.1(watu milioni 3.5) na majumbani asilimia 13.8 (watu milioni 4.1)," alisema.

Waziri Ummy alisema utafiti huo una umuhimu wa kipekee katika wizara, kwa kuwa matokeo yake yatasaidia kutathmini hatua zilizofikiwa katika kupambana na magonjwa makuu manne yasiyoambukiza ambayo ni saratani, magonjwa ya moyo, magonjwa ya mfumo wa hewa na kisukari.

Aliagiza watendaji wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wadau wengine, kutengeneza au kupitia upya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku, ili iendane na Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yake.

Pia, aliitaka Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha wale wanaokiuka miongozo kama vile kuendelea kuvuta sigara kwenye maeneo ya wazi, wanachukuliwa hatua stahiki.

"Watengenezaji na wauzaji wa sigara wafuate miongozo iliyowekwa na serikali ikiwamo kutokuweka mabango au kutangaza na kuhamasisha matumizi ya sigara, kupitia bidhaa kama miamvuli, T-Shirts, kofia na kutowauzia watoto wenye umri chini ya miaka 18," alisisitiza.



Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Janeth Masaburi (kulia), akikabidhi msaada wa kompyuta tano na printa moja kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ihumwa, Greyson Maige, jijini Dodoma juzi, kwa ajili ya matumizi ya kufundishia shuleni hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hospitali ya Benjamin Mkapa kujenga mtambo wa oksijeni

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH), imepanga kujenga mtambo wa kuzalisha gesi ya oksijeni kwa ajili ya huduma za matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, aliyasema hayo jana alipotoa taarifa yake kwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, aliyetembelea hospitali hiyo ikiwa ni sehemu ya ziara yake kutembelea hospitali za umma.

Dk. Chandika alisema kuanza kwa mtambo huo kutapunguza tatizo la uhaba wa gesi ya oksijeni katika huduma za matibabu Kanda ya Kati na mikoa jirani, akibainisha kuwa kwa sasa wanategemea huduma hiyo kutoka kwa msambazaji mmoja pekee.

"Tumekwishawasilisha andiko la mradi wizarani na ni matarajio yetu kuwa gesi tutakayoizalisha tutaitumia sisi wenyewe kwenye huduma zetu za tiba, lakini pia tutasambaza katika hospitali nyingine zitazohitaji huduma hiyo," alisema.

Dk. Chandika alisema oksijeni inatumika kwa wagonjwa katika vyumba vya upasuaji hospitalini na katika mashine za kusaidia upumuaji.

Akizungumzia mradi huo, Naibu Waziri Dk. Mollel alieleza kufurahishwa na wazo hilo na kuahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kuuanikisha.

Dk. Mollel alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa BMH kwa jitihada anazozifanya kuimarisha huduma za afya katika hospitali hiyo ya umma na kuwaomba watumishi wa hospitali hiyo kuendelea kumpa ushirikiano mkurugenzi huyo katika utekelezaji wa majukumu yake.

## Mbunge awaomba wadau kuisaidia serikali kuboresha sekta ya elimu

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), ameziomba taasisi na watu binafsi kuendelea kuiunga mkono serikali kwa kutoa michango ya kuwahudumia wananchi kwenye sekta ya elimu.

Janeth Masaburi alitoa rai hiyo jana alipokabidhi msaada wa kompyuta kwenye Shule ya Sekondari Ihumwa jijini hapa.

Aliziomba taasisi, watu binafsi na mashirika kuendelea kuiunga mkono serikali katika kuwahudumia wananchi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo na elimu kwenye maeneo yao.

"Serikali inafanya kazi nyingi za kutuletea maendeleo, hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha tunaiunga mkono kwa kuendelea kuchangia maendeleo ya elimu na mengine," alisema.

Masaburi alisema msaada huo aliokabidhi kwa shule hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano katika kuwahudumia walimu na wanafunzi kujifunza kwa njia ya kiteknolojia.

"Mliniomba msaada wa kompyuta tangu mwaka jana na nilizinunua kompyuta hizi, na ilikuwa nizikabidhi Machi mwaka huu, lakini kutokana na ugonjwa wa corona, ilinibidi nisubiri hadi leo (jana) nimezileta rasmi, ninaomba mzipokee," alisema.

Alitaja baadhi ya vitu alivyokadhi kuwa ni kompyuta tano za kisasa na printa moja, akitaka ziwe chachu ya maendeleo ya elimu katika shule hiyo.

Alisema msaada huo umetokana na wadau wengine wa maendeleo aliowaomba wakiwamo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) pamoja na wadau wengine wa maendeleo nchini.

"Kama mnavyojua, mimi ni Mbunge wa Kuteuliwa na Rais, mimi sina jimbo, ninafanya kazi na watu wote nchi nzima, hapa nimeleta kompyuta tano, lakini zingine nimepeleka kwenye shule zingine kwa lengo hilo la kuunga mkono juhudi za serikali kuleta maendeleo," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ihumwa, Greyson Maige, alimshukuru mbunge huyo kwa msaada huo na kuahidi kuzitumia kwa ajili ya kufundishia wanafunzi shuleni huko.

"Msaada huu umekuja wakati mwafaka, shule yetu hatuna kompyuta hata mmoja, zilizopo ni za kuazima, tuliomba kwa ajili ya kuwatumia masomo wanafunzi wakati huu wa mapumziko, lakini leo kompyuta hizi zitaanza kutumika kwa ajili kuandaa masomo kwa wanafunzi wetu," alisifu.

Alibainisha kuwa shule hiyo ina wanafunzi 782 walimu 44 na pia kuna kikwazo cha miundombinu ya kuingia shuleni.

# Z'bar yadhibiti corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema imefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa corona kwa kubaki na wagonjwa 10 pekee wanaopata huduma za afya katika vituo vya Unguja na Pemba huku vituo vinne vikifungwa baada ya kukosa wagonjwa kwa zaidi ya wiki mbili.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, alisema hayo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2020-2011 katika Baraza la Wawakilishi Chukwani nje kidogo ya mji wa Unguja.

Alisema hadi sasa kuna wagonjwa 10 waliolazwa katika vituo vinavyotoa huduma za wagonjwa hao wakati Pemba kuna mgonjwa.

Alisema baadhi ya vituo vilivyokuwa vikitoa huduma za wagonjwa hao tayari vimefungwa baada ya kukosa wagonjwa wa aina hiyo.

''Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Baraza la Wawakilishi kwamba, tumepata mafanikio makubwa katika kudhibiti na kupambana na ugonjwa wa corona, kwa sasa wapo wagonjwa 10 wanaopata matibabu katika vituo vinavyopokea wagonjwa hao wakati kwa upande wa kisiwa cha Pemba yupo mgonjwa mmoja," alisema.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na mwongozo na maelekezo yaliyokuwa yakitolewa na viongozi wakuu wa nchi akiwamo Rais John Magufuli pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ikiwamo kuwatoa hofu na wasiwasi wananchi kuhusu ugonjwa huo.

Aliwataka wananchi kuendelea kufuata masharti ya afya kujikinga na ugonjwa wa corona ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na sababu pamoja na kuvaa barakoa na kusafisha mikono kwa kutumia vitakasa mikono.

Alisema serikali itaendelea kulegeza masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo hatua kwa hatua katika siku za hivi karibuni.

Pia, alisema serikali imetoa ruhusu kufunguliwa kwa vyuo vikuu pamoja na shule za sekondari kidato cha sita kwa ajili ya matayarisho ya mitihani ya taifa.

"Hali ni nzuri pengine tunaweza kuruhusu baadhi ya mashirika ya ndege kuja nchini kwa ajili ya kuleta watalii," alisema.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Said Hassan (kushoto), akiteta jambo na Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati, Salama Aboud Talib, wakiwa nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi wampongeza JPM, Dk. Shein kwa ujasiri

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamewapongeza viongozi wakuu wa nchi akiwamo Rais John Magufuli pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutoa miongozo na maelekezo iliyosaidia kudhibiti ugonjwa wa corona na kupunguza maambukizo nchini.

Mwakilishi wa jimbo la Shaurimoyo, Hamza Hassan Juma, alisema ugonjwa wa corona ulichangiwa na hofu waliyokuwa nayo wananchi ambayo ilipunguzwa kwa kiasi kikubwa na Rais John Magufuli aliyekuwa akiwatia moyo na kusema ugonjwa huo utadhibitiwa na kuondoka katika siku za hivi karibuni na shughuli za wananchi kuendelea.

Alimpongeza Rais Magufuli ambaye alipuuza kauli zilizokuwa zikitolewa na wapinzani waliotaka wananchi wafungiwe ndani kama njia muafaka ya kujilinda na ugonjwa wa corona kwa kutaka kuiga mataifa mengine ya jirani.

"Tunakupongeza kwa dhati Rais Magufuli pamoja na Rais Shein kwa kuwapuuza wapinzani waliokuwa wakitaka wananchi wafungiwe ndani kama njia muafaka ya kupambana na ugonjwa wa corona...uongozi wenu wa busara tumeuona," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulatfif Yussuf, alisema mafanikio makubwa yoliyopatikana katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona yanatokana na maelekezo ya viongozi wao ambao walikataa kusikiliza ushauri mbaya kutoka kwa watu ambao hawaitakii mema nchi.

Alisema yapo mataifa ya nje yaliyokuwa yakiwashinikiza viongozi hao kuwafungia wananchi kama njia za kupambana na ugonjwa wa corona, lakini kwa bahati nzuri Rais Magufuli pamoja na Rais Shein msimamo wao imara ulitosha kudhibiti maambukizo mapya.

"Viongozi wetu wameshinda katika vita mara mbili kwa sababu walikuwa wakipambana na corona, lakini pia walikuwa wakipambana na maadui wapinzani ambao walikuwa wakitumia ugonjwa huo kutaka kujikweza kisiasa," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Wawi Pemba, Hamad Abdalla Rashid, alisema viongozi wa mikoa miwili ya kisiwa hicho kuendelea kudhibiti uingiaji wa watu kutoka nje ya visiwa hivyo kama njia moja wapo ya kudhibiti ugonjwa wa corona.

Alisema kisiwa cha Pemba kimepakana na mikoa mingi ikiwamo ya Tanzania Bara pamoja na Mombasa Kenya, hivyo tahadhari zaidi za maeneo ya mipakani zinahitajika kuchukuliwa licha ya kuwapo nafuu kubwa ya kupungua maambukizo.

"Tumepunguza maambukizo ya ugonjwa wa corona, lakini kamwe tusibweteke, mikakati ya kudhibiti uingiaji wa watu pamoja na kuwapima unatakiwa kuendelea kuchukuliwa," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu, Amina Mabruki Iddi, alisema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajivunia kwa kuwa na viongozi hazina wenye busara na uamuzi wake siku zote ni wa hekima.

"Nawapongeza kwa dhati viongozi wetu, Mungu awape maisha marefu na busara na hekima katika uamuzi wao...leo hii tunashuhudia Bara na Zanzibar wagonjwa wa corona wamepungua sana," alisema.

Tayari vituo vitatu vilivyokuwa vikitoa huduma za wagonjwa wa corona katika kisiwa cha Pemba vimefungwa na kubakia na kituo kimoja pekee cha Vitongoji kilicho na mgonjwa mmoja.

## SMZ kuendelea kutoa matibabu bure

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amesema mikakati na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ni kuendelea kutoa matibabu bure ikiwa ni kutekeleza azma na dhamira ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoasisiwa na Rais wa kwanza hayati Abeid Amani Karume.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964, yalikuwa kuwapatia wananchi huduma muhimu za kijamii ambazo zilikosekana katika kipindi cha utawala wa kisultani ikiwamo elimu, matibabu, pamoja na ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo na makazi.

"Mimi katika kipindi chote nilichokuwa waziri nilikuwa na majukumu ya kutekeleza sera za Chama cha Mapinduzi zinazotokana na Ilani ya CCM, ambayo ni kuwapatia wananchi matibabu bure ya aina zote yanayopatikana nchini," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka 10 ya uongozi wa Rais Ali Mohamed Shein, huduma za afya zimeimarishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo jumla ya wagonjwa 64 wenye matatizo ya figo wamepatiwa huduma za kusafisha damu.

Pia, jumla ya wagonjwa sita walipandikizwa figo na huduma za wagonjwa wa saratani wapatao 221 wakipatiwa matibabu ya aina mbalimbali na wagonjwa wa huduma za moyo wapatao 1,646 wamehudumiwa.

"Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi ya matibabu makubwa yanayopatikana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, yakitolewa bure kwa wananchi wetu ikiwa ni sehemu ya kutekeleza mikakati ya matibabu bure kwa wananchi wote," alisema.

Aliitaja mikakati mikubwa inayotekelezwa na Wizara ya Afya kwa sasa kuwa ni pamoja na ujenzi wa maabara ya kisasa ya kuchunguza maradhi mbalimbali, inayotarajiwa kujengwa huko Binguni.

Alisema serikali katika mwaka wa fedha 2020-2011 imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa hospitali ya kisasa ya rufani huko Binguni, Wilaya ya kati Unguja.

"Hiyo ndiyo miradi mikubwa ya kimkakati katika Wizara ya Afya ambayo imepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020-2011 kwa lengo la kuimarisha huduma za afya na kuzifanya kuwa bora zaidi," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2020-2011.



**DAVIDO HATAKI UTANI, MAISHA YAKE YAPO JUU** Uk. 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 6, 2020



## NANDY

# Billnas sijampenda kwa macho wala umbo, ila...

HATIMAYE Mwanamuziki nyota wa kike Afrika Mashariki, Nandy, ameamua kuanika moyo wake hadharani baada ya kusema huwa anaweweseka pale anapomuona mchumba wake Billnas

Nady, amesema hajajua kitu gani anachofurahishwa nacho, lakini anashangaa kila anapumuona anabadilika na kuweweseka kwa furaha, kama makinda ya ndege yanapomuona mama yao.

"Ukweli sijajua ni kitu gani nakipenda kwa Billnas, lakini najikuta tu nakuwa na furaha kupita kiasi pale ninapomuona na jambo hilo huwa nalishangaa," amesema Nandy.

Aidha, ameeleza wapo wanawake wanaosema wanampenda mwanaume kutokana na vitu mbalimbali kama macho, umbo, mwendo au tabasamu, lakini kwake ni tofauti kwani hana kitu ambacho anaweza kukizungumzia.

"Wote tunapendana sana, lakini siwezi kusema nampenda kutokana na macho, miguu au umbo, itoshe kwamba nimerishika naye," akaongeza.

Ameeleza uhusiano wao ulianza muda mrefu na hata walipoachana, walibaki kuwa marafiki wa karibu.

"Nakumbuka wakati ule tulipoachana tukiwa kama marafiki, aliniambia kama tukirudiana itakuwa ndoa moja kwa moja. Suala la kunivisha pete sikufahamu alinishtukiza tu," Nandy amezidi kusema.

Pamoja na furaha aliyonayo, Nandy ameeleza anachukia maisha ya kutokuwa na faragha, kwani kila kitu anachokifanya kinafuatiliwa na wakati mwingine anapata wakati mgumu kutokana na mashabiki wake kutomvumilia.

**BASI SAWA**

## Mabeste sikia ushauri huu

MASHABIKI wa msanii Mabeste, wamemshauri kukaa kimya kwani anapolalamikia mapenzi yaliyopita ni sawa na kujishusha.

Ushauri huo wameutoa baada ya msanii huyo kuitwa kituo cha Polisi Oysterbay, akidaiwa kumchafua mitandaoni mzazi mwenziye na mkewe wa zamani Lissa.

"Imefikia wakati mabeste anatakiwa kuacha kuzungumzia mapenzi yake ya zamani, tunajua ameumizwa lakini ni lazima akubaliane na matokeo kwani kuendelea kulalamika sawa na kujishusha kwamba hawezi kumpata mwingine," amesema shabiki mmoja.



## Shilole atakaza vita kwa Uchebe

KUMEKUCHA! Mwanamuziki wa Bongo Fleva, Shilole, ameapa kufa na mtu endapo atagundua kuna mwanamke anamnyemelea mume wake Uchebe.

Akizungumza kupitia kipindi cha Planet Bongo cha East Africa Radio, Shilole amesema hata kama ndoa ni kuvumiliana kwenye raha na shida, lakini hawezi kukaa kimya kama akigundua kama mumewe ana mwanamke mwingine.

"Tutatafutana Jerusalem, sisemi uongo na raundi hii nikijua naua mtu, kama anafanya mambo yake afanye huko mimi nisijue, kwani nani asiyejua kwamba Shilole mumewe ni Uchebe? Alihoji Shilole.






## Thea ndani ya 'Ndoa Yangu'

MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Ndumbayo Misayo, maarufu kama "Thea", anakuja kivingine baada ya kufanikiwa kuanza kurusha tamthilia kupitia vituo mbalimbali vya Runinga.

Tamthilia hiyo inayoitwa 'Ndoa Yangu' inayowakutanisha mastaa tofauti, inaonekana kwenye ving'amuzi vya MamboTVswahili, Stertimes na Zuku.

Ndani ya tamthilia hiyo unayozungumzia maisha ya ndoa, uhusiano, usaliti, malezi na familia, inawakutanisha wasanii ..

Ambapo ndani kuna Suzan na Denis wanaingia katika uhusiano wa ndoa kila mmoja akiwa na mtazamo wake.






## Hamisa hayajakukuta, wenzio wanakuangalia tu

MWANAMITINDO na msanii wa muziki nchini, Hamisa Mobetto, amesema kamwe hatishwi na baadhi ya wanawake wenye tabia ya kunyuakua waume za watu.

Akizungumza na ETV, Hamisa amefafanua kwa sasa yupo kwenye uhusiano na mwanaume ambaye hataweza kumtambulisha kwa sasa hadi hapo atakapoolewa.

"Nipo kwenye uhusiano, sidhani kama naweza nikaogopa manyakunyaku, katika vitu ambavyo naweza nikaviogopa vipo vingi lakini sio mwanamke kunichukulia mwanaume wangu, kama akiamua kuondoka ni mipango ya Mungu na hakupangwa kuwa wangu," amesema Hamisa.



## Ngoma 5 zilizobamba mwezi Mei

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni mwezi wa sita na tayari mwaka 2020 umegawanyika mara mbili. Mwezi Mei haukuwa mzuri sana kutokana watu kuishi kwa wasiwasi kutokana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Lakini pamoja na mambo yote, watu waliendelea na maisha yao ya kujipatia kipato kama kawaida. Vile vile kwenye masuala ya burudani, wasanii walikuwa wakiingia studio kutoa ngoma ambazo zimekuwa zikiwaliwaza hasa kutokana na kipindi hiki kigumu.

Leo tunawaletea ngoma ambazo zimetoka mwezi Mei na kutamba kwenye mitandao ya kijamii, redio, televisheni, huku zikikonga nyoyo za mashabiki wengi nchini.

**TUCHATI-ROSTAM**

Hadi tunaandika hapa, tayari ngoma hii ilikuwa imeshatazamwa na watu milioni mbili, laki nne na ushehe hivi. Ni ngoma iliyotoka Mei 9, ikiwa ndiyo ngoma bora zaidi kutoka na kupendwa na mashabiki wengi wa muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania.

Wasanii waliotoa ngoma hii ni Roma Mkatoliki na swahiba yake Stamina. Mmoja yuko nje ya nchi, mwingine yuko nchini na unavyoimbwa na maudhui yake, ni kama watu wanaolizana juu ya mambo mbalimbali yanayoendelea huko waliko, ikiwemo pia suala ya ugonjwa corona.

**ONE NIGHT STAND-IBRAAH FT HARMONIZE**

Ni ngoma ya mapenzi, iliyoimbwa na msanii Ibraah, lakini akamshirikisha msanii maarufu nchini Harmonize na kuifanya ikubalike na kuteka hisia za mashabiki wengi nchini kiasi cha kila kona unayopita, huwezi kukata mitaa miwili mitatu usiisikie. Kwenye mtandao wa kijamii, tayari imeangaliwa na mashabiki milioni tatu na laki mbili tangu ilipowekwa Mei 12.

**RAHA-ZUCHU**

Mei 4, msanii wa kike ambaye kwa sasa amekuwa gumzo kutokana na kipaji cha hali ya juu alichokuwa nacho, Zuchu, alitoa ngoma yake aliyoiita 'Raha'.

Tayari imetazamwa na mashabiki milioni moja na laki moja mpaka sasa kwenye mtandao wa kijamii na kuwa moja ya ngoma bora sana mwezi uliopita.

**SIMU-GOODLUCK GOZBERT**

Ngoma ya 'Simu' ilitoka Mei 11, msanii akiwa ni Goodluck Gozbert. Maudhui ya wimbo huu ni musuala la corona. Alilamika vitu vingi, ikiwemo baadhi ya uzushi wa baadhi ya watu wanaotangaza wagonjwa wanaoumwa na kufa, kana kwamba wao ni madaktari.

Falling in Love-Harmonize

Msanii Harmonize ni kama ameufunga mwezi Mei, kwani siku tano kabla ya kuuaga mwezi wa tano, Yaani Mei 26, akatoa ngoma moja kali aliyoiita 'Falling in Love.'

Wimbo huu umeimbwa kwa lugha ya kiingereza, na kwa muda huu mfupi tu tangu utoke umeshatazamwa na watu kiasi cha milioni moja kwenye mtandao wake wa kijamii.

## Matilda: Duniani chochote kinawezekana

**Na Adam Fungamwango**

HAPA duniani chochote kinawezekana. Unaweza kuona kama kuna kitu fulani si rahisi kufanyika kutokana na mazingira yaliyopo, lakini ukweli ni kwamba hakuna ambacho kinashindikana.

Ndiyo maana wapelelezi na watu wa intelejensia siku zote wanamsemo kuwa, usiamini kitu chochote au mtu yoyote, hata kama ni maiti.

Na ukitaka kuamini hilo, hebu ifuatilie hii filamu ya 'Matilda'.

Imechezwa na baadhi ya wasanii mbalimbali maarufu kama Mzee Jengua, Salma Jabu 'Nisha', Wellu Sengo, Hemed Suleiman, Kikumba na wengine wengi.

Nisha ni mfanyakazi wa kampuni moja binafsi, anapata matatizo ya kushindwa kulipa kodi, kitu kinachosababisha kumuomba Hemed ambaye anaelewana naye, amsaidie kwa bosi.

Hemed anafanya hivyo na bosi anampa hiyo pesa kwa ajili ya kodi. Lakini wakati Nisha anaondoka anapewa lifti na bosi, ambaye anataka kutumia msaada huo kuomba penzi.

Badala ya Nisha kupelekwa kwake, anapelekwa nyumbani kwa bosi wake na kuomba penzi kinguvu. Nisha anakimbia, na ikawa kama amejichongea kwani kesho yake tu akapewa barua ya kuachishwa kazi.

Anaporudi nyumbani anakuta tayari ameshatolewa vitu nje, wapangaji wenzake wakimsindikiza kwa maneno ya kejeli.

Nakwambia aliondoka na mdundiko, matarumbeta nyuma. Alichofanya ni kumpigia Hemed ambaye alimtaka aende kwake. Huko alipata hifadhi. Pamoja na kuishi hapo, Hemed hakushawishika na Nisha, badala yake akaangukia kwenye penzi na msichana mwingine mcheza shoo aitwaye Matilda.

Hata hivyo, wazazi wa Hemed wao walivutiwa mno na Nisha na kumlazimisha kijana wao amuoe, lakini ilishindikana.

Kilichotokea ni kwamba Hemed alimpa mimba Nisha na kumkimbia kwenda kupanga nyumba nyingine, akaishi na Matilda.

Nisha anafukuzwa kwenye nyumba kwa kukosa kodi, anaingia mtaani na kuanza kubangaiza, akifanya biashara ya kuuza vitumbua, akilea mimba yake, hadi alipojifungua.


Maisha ya Hemed na Matilda yalikuwa kama ya maigizo. Mara anatoroka kwenda kwenye kazi zake za shoo, wakati alishakatazwa. Mara anachukua simu ya mumewe na akikuta namba za wanawake, anawatukana. Siku moja akamtukana bosi mmoja wa kike wa kampuni yao, akidhani ni mmoja wa maharawa zake. Hiyo ilitosha Hemed kufukuzwa kazi. Ukazuka ugomvi mkubwa baina yao na kusababisha Matilda akasirike na kumchukua mtoto usiku kuondoka naye.

Njiani anakutana na watu wabaya, wanambaka. Mtoto anapotea, lakini akaanguka kwenye mikono ya Nisha ambaye naye ana mtoto wa Hemed.

Matilda anasaka mtoto na kufanikiwa kumpata akiwa kwenye mikono ya Nisha. Katika kuulizana wanajikuta wanafahamiana kuwa ni mtu na dada yake wa baba na mama mmoja.

Wote wamezaa na Hemed kila mmoja mtoto mmoja wa kiume.

Matilda baada ya kubakwa anapimwa na kukuta ana maambukizo ya ukimwi, hivyo anamchukua mdogo wake Nisha na kumpeleka kwa Hemed, akimwambia kuwa amuoe badala yake, ili alee watoto. Matilda anajiua kwa kunywa sumu.





# Davido hataki utani, maisha yake yapo juu

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria, Davido, anaendelea kufurahia maisha baada ya kuhamia katika jumba lake la kifahari katika kisiwa cha watu matajiri cha Banana.

Kisiwa hicho cha kutengenezwa kipo katika jiji la Logos, kinakaliwa na watu maarufu na wenye fedha, hivyo Davido, amekuwa na furaha zaidi kuishi eneo hilo lenye kila aina ya sifa.

Nyumba ambayo aliiposti katika mitandao ya kijamii, imeonekana kuwa ya kifahari zaidi na kusababisha mashabiki wake kuhoji kama ameinunua au amepanga.





## Wizkid utamfananishaje Buhari na Trymp?

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Wizkid, amemcharukia Rais Muhammadu Buhari, akidai hana matumaini katika maswala mbalimbali yanayoisumbua nchi hiyo.

Katika ukurasa wake wa twitter, Wizkid, alimfananisha kiongozi huyo sawa na Rais wa Marekani,Donald Trump, kwa maono yao yasiyoelweka.

"Buhari na Trump watu hawana utofauti, hana matumaini katika kile anachozungumza kuhusu Nigeria," ameandika msanii huyo.

## Tangulia Fashek, umemaliza ya dunia

MASHABIKI wa muziki nchini Nigeria, wanaendelea kuomboleza kifo cha msanii mkongwe, Majek Fashek, ambaye amefariki siku ya Jumanne ya wiki hii.

Fashek, ambaye alifahamika tangu mwaka 1988 single ' kwa wimbo wake maarufu "Send Down the Rain' amekuwa alama ya muziki wa nchi hiyo.

Badhi ya mashabiki waliingia katika mtandao wa Twitter, wakielezea namna walivyoguswa na msiba huo ambao umwewaacha katika majonzi mazito.





## Da! Kumbe Kylie 'aliwafiksi' Forbes

JARIDA maarufu la Forbes, ambalo linaaminika kwa kutaja utajiri wa watu mbalimbali maarufu, limeibua tuhuma nzito kwa mwanamitindo, Kylie Jenner, kuwa alitoa taarifa feki ya mali zake.

Katika mtandao wa jarida hilo, lilisema nyota huyo wa kipindi cha maisha katika Runinga, ametoa orodha hewa ya mali zake ili kujinufaisha binafsi.

Ikaongeza "Biashara ya Kylie kwa ujumla ni ndogo na faida yake haitoshi kwa matumizi ya familia yake kwa miaka katika vipodozi na sekta ya habari kama Forbes, ilivyoaminishwa."

Hata hivyo, Kylie, amesema ameamua kuweka umakini katika mambo mengine muhimu kwake kuliko suala hilo.

## Unga umewaondoa Boyce, mpenzi wake Natalie

MWIGIZAJI kutoka Hollywood, Gregory Boyce, na mpenzi wake Mnigeria, Natalie Adepoju, wamekufa baada ya kuzidisha kiwango cha dawa za kulevya.

Kulingana na mtandao wa PageSix, katika ripoti ya uchunguzi, imesema wawili hao walipoteza maisha muda mfupi baada ya kutumia dawa aina ya cocaine.

Boyce ambaye anafahamika kama Tyler Crowley, na Matalie walikutwa wamefariki ndani ya nyumba yao jijini Las Vegas.



MAKALA

# HakiElimu yaanika utafiti wake unaofukua kikwazo elimu awali

## ■ Dk. Kalage: Shida kuu iko hapa

**Na Mwandishi Wetu**




Wanafunzi wa Shule ya Awali ya Mchangani, jijini Dar es Salaam, walipoonyesha bango lenye ujumbe wa kuboreshwa elimu ya awali. **PICHA ZOTE: HAKIELIMU.**

ELIMU ya awali au Chekechea ni mwanzo wa maendeleo ya mtoto kitaaluma. Ni sehemu ya makuzi na maendeleo yanayoanzia tumboni mwa mama hadi umri wa elimu msingi.

Pia, ni muhimu kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), kipengele kinachoshurutisha mataifa duniani ifikapo mwaka 2030, yawe yameshapatia watoto makuzi, ulinzi na elimu bora ya awali, ikiwaandaa kwa elimu ya msingi.

Katika hilo, asasi ya HakiElimu imekuwa mtetezi na muelimishaji kwa kushirikiana na serikali na wadau, kuhakikisha mtoto Mtanzania ana haki hiyo, akiandaliwa vyema kijunga na elimu ya msingi, baadaye awe raia bora.

Haki Elimu hushiriki kushawishi utungaji na utekelezaji sera bora za mtoto na elimu, uelimishaji na uhamasishaji umuhimu wa elimu na makuzi ya mtoto.

Pia, inaangalia juhudi za jamii kujenga madarasa na uboreshaji mazingira ya kujifunza; uhamasishaji ulinzi wa mtoto shuleni na nje ya shule.

Mwaka jana ilifanya utafiti mara mbili kujifunza kwa kina katika eneo hilo, mtazamo wa jumla ni kuangaza mahitaji ya awali ya mtoto nje na ndani ya mfumo rasmi wa elimu nchini,

Utafiti wa kwanza uliangaza namna bora ya kujumuisha ulinzi wa mtoto katika elimu ya awali; wa pili kujifunza na ufundishaji wa elimu ya awali nchini.

**MKURUGENZI**

Mkurugenzi wa HakiElimu, Dk. John Kalage, anasema malengo makuu ya utafiti ni kujifunza na kuonyesha hali halisi ya umuhimu wa nchi kuzingatia kumlinda mtoto.

Pia, anataja utambuzi wa uelewa, mtazamo wa wazazi, jamii na walezi wa watoto wanavyozingatia ulinzi na maendeleo ya wadogo hao, pia changamoto ya makuzi yao.

Sura nyingine anaitaja ni kukagua elimu ya awali nchini. Hapo HakiElimu ilizama kudodosa uandikishaji watoto, kuzingatia hali ya ulemavu, jinsia, umri na jiografia ya wanakoishi .

Dk. Kalage anasema walidadisi ufundishaji na upatikanaji wa elimu kwa watoto hadi umri miaka sita, wakiangalia ushirikiano kati ya walimu, wazazi na jamii kunakomhakikishia mtoto elimu bora.

Anafafanu, walifuatilia uelewa na utayari wa walimu wa madarasa ya awali kuwaelimisha na malezi yanayozingatia mahitaji na uwezo wa kila mtoto

Dk. Kalage anasema, HakiElimu imejifunza kuwapo mambo taifa inapaswa kuzishughulikia mtoto nchini awe salama, makuzi na elimu bora katika umri chini ya miaka sita.

Anatoa mfano wa ufafiti unaoangaza Tanzania kupitisha sheria na miongozo inayolenga kumlinda mtoto tangu tumboni mwa mama yake, hadi umri wa kujitegemea miaka 18 (Katiba ya Tanzania, 1977).

Hapo, ndipo inaangukia sheria za kuzuia utoaji mimba isipokuwa inalazimika kiafya kwa mujibu wa ushauri wa daktari.

Baada ya kuzaliwa, Sheria ya Mtoto na miongozo mingine ya kiafya inatoa ulinzi unatamka haki za wazazi, walezi na jamii kuwajibika: Uhai, kutonyanyaswa, huduma muhimu, chakula, matibabu, malazi na elimu.

**UANDIKISHAJI ULIVYO**

Kwa mujibu wa Dk. Kalage, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2008 na Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, zinatoa haki mtoto aelimishwe, ikianzia na darasa awali ambayo ni lazima, wazazi, walezi na jamii wanawajibishwa, pia elimu msingi ambayo ni ya lazima.

"Kwa miongozo hii, takribani kila shule ya msingi Tanzania ina walau darasa la awali ambalo linafanya kazi ya kuwapatia elimu watoto wetu," anasema, akigusia mafanikio asilimia 99.6 ni kwa shule zote nchini walikozuru.

Pia, anakiri uandikishaji watoto madarasa ya awali uko vizuri kwa zaidi ya asilimia 100, ikilinganishwa malengo yaliyowekwa kitaifa, akirejea wilaya nane utafiti ulikofanyika.

**CHANGAMOTO**

Dk. Kalage anataja changamoto kutoka makundi ya watoto wenye ulemavu, wenye mazingira magumu na wafugaji, uandikishaji umebaki chini ya asilimia 70 ya malengo.

Pia, kuna suala wastani waa utoaji mimba 36 kwa kila wanawake 1000 (asilimia 3.6) wanaopata ujauzito, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti kutika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Chuo Kikuu - Muhimbili, mwaka 2016.

Eneo lingine analitaja ni kuongezeka unyanyasaji watoto, kukosekana ulinzi na huduma, idadi kubwa ya watoto wasiokuwapo masomoni wanataabika kimazingira.

Wilaya zote zilizofanyiwa utafiti zinaonyesha changamoto kwa watoto hao kuhusu uhaba wa miundombinu masomoni kama vile vyoo, madarasa, maji safi, lishe shuleni, madawati, mahali salama pa kucheza na vifaa vya michezo.

Dk. Kalage anasema utafiti unaanika uhaba wa walimu wenye sifa katika madarasa ya awali kwenye shule zote walizopitia.

Pia, takwimu za kitaifa za hali ya walimu wa awali (BEST 2018), kila mwalimu mmoja mwenye sifa anahudumia wanafunzi 114 (1:114), badala ya 25 (1:25) kama inavyotakiwa na miongozo ya elimu.

Inaelezwa nusu ya walimu wa madarasa ya awali walioshiriki utafiti hawana uelewa sahihi wa maana ya elimu ya awali na mahitaji yake na wanafundisha katika mfumo sawa na elimu ya msingi, kinyume na stadi rasmi zinazoshauriwa kitaalamu

Dk. Kalage anakumbusha mijadala inayohusu uhalisia wa elimu iambatane na janga la maradhi corona, kwani zinahusiana na elimu ni mwathirika mkuu, hivyo mtoto anayelindwa ana haki ya kutaafiriwa.

**WALIMU WASEMA**

Katika uzinduzi wa utafiti, Mwalimu Joyce Kiango, anataja changamoto wanazopata walimu wa awali ni ushirikiano mdogo kutoka kwa wazazi na wadau, hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu au wanaoishi mazingira magumu.

Mwalimu Kiango anatumia mfano wa kuwapo mzazi anayemleta mtoto shuleni bila ufafanuzi wa matatizo yake kiafya, hivyo linakuwa limejificha, inaishia kwa mwalimu anashindwa kufanikishia malengo yake kimasomo.

Rai yake, ni wazazi watoe ushirikiano kila wanapowapeleka watoto shuleni, ili matatizo yao yajulikane ili mwanafunzi asaidiwe masomoni. Ni changamoto iliyobainika pia kwenye utafiti.

Matokeo ya ushirikiano duni kati ya wazazi na walezi, yamechangia watoto kukosa mahitaji ya msingi kama vile lishe na wanakumbwa na unyanyasaji, kwa kutopata ulinzi unaojitosheleza.

Dk. Kalage anapendekeza kuwapo uandikishaji wa watoto wanaoishi na ulemavu na waishio kwenye mazingira magumu ili wajulikane, ikizingatiwa wako wachache.

Mwalimu Richard Mabala, anasema shule za awali zinawasaidia sana wazazi mjini, hasa waajiriwa ofisini (hata wenye shughuli mijini na vijijini) na mabinti wanaoajirwa majumbani kuwahudumia, hawamudu matakwa ya kuwahudumia .

Mabala anashauri kuboreshwa elimu hiyo, kuanzia kwa walimu, mazingira ya kufundishia na vifaa, ili kukidhi matakwa ya kujifunza, kucheza na malezi yatakayowajenga watoto kiakili.

Anasema kuna hali tofauti na mazingira ya malezi, elimu ya awali kwa watoto wanaoishi katika baadhi ya maeneo vijijini hasa kwa jamii za wafugaji, watoto wadogo hupatiwa elimu isiyo rasmi kutoka kwa wazazi, hivyo serikali na wadau wanapaswa kuweka mkazo kufanikisha mageuzi.

Mwalimu Mabala, anakumbusha umuhimu wa kuhamasisha na kuongeza mafunzo na ajira kwa walimu wa elimu ya awali.



Mkurugenzi wa HakiElimu, Dk. John Kalage.

# TBS kupitia Maabara Ugezi inapodhibiti viwango vya vipimo kuwalinda walaji

**Na Mwandishi Wetu**



Ukaguzi wa mizani njia mojawapo inayotumika kujua kama ina uhalali wa matumizi ya kila siku.

MEI 20, mwaka huu Tanzania imeungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Vipimo Duniani (World Metrology Day). Mataifa mbalimbali duniani hushiriki kwa namna tofauti kuadhimisha siku hii muhimu.

Chimbuko la Siku ya Vipimo Duniani ni kumbukumbu ya kusainiwa kwa Mkataba wa Mita (Metre Convention) ambao makubaliano yake yalisainiwa na mataifa 17, Mei 20, 1875.

Mkataba wa Mita uliweka mazingira sahihi ili kuwezesha dunia kushirikiana katika masuala ya sayansi ya vipimo na matumizi yake katika viwanda, biashara na jamii.

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya kuona kila nchi ina vipimo vyake, hivyo mataifa hayo yaliona mataifa yote yawe na vipimo vinavyofanana, yaani ukipima kilo moja ya sukari au unga, lazima ukienda Afrika Kusini au China iwe inafanana.

Lengo hasa la mkataba wa mita ni kuhakikisha kuwa duniani kote vipimo vinafanana, hatua ambayo ililenga kuondoa mkanganyiko wa matumizi ya vipimo visivyofanana.

Katika mkataba huo nchi zilikubaliana suala zima la kutumia vipimo vya aina moja. Kwa mantiki hiyo hakuna nchi inayoweza kufanya vipimo bila kufuata mfumo uliokubaliwa. Mkataba huo ulikubaliana suala zima la kuwa na vipimo vya aina moja.

Kimataifa, siku ya Vipimo Duniani huandaliwa na kudhaminiwa na taasisi mbili, International Bureau of Weights and Measures (BIPM) na International Organization for Legal Metrology (OIML).

Tanzania imeshiriki maadhimisho hayo kupitia Maabara ya Ugezi ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu imebeba ujumbe usemao; "Vipimo katika Biashara za Kimataifa."

Mkuu wa Maabara ya Ugezi iliyo chini ya TBS, Joseph Mahilla, anasema wao ni wadau wa vipimo kupitia Maabara ya Ugenzi kwa sababu ndiyo mtunzaji Vipimo vya Taifa, kwa maana hiyo vipimo vya Tanzania vinatunzwa TBS.

Mahilla, anasema Maabara ya Ugezi ilianzishwa mwaka 1982 ili kuwasaidia wazalishaji kuongeza ubora wa bidhaa zao, kwa kuzingatia viwango vilivyo nchini au vya kimataifa lengo kuu likiwa ni kumlinda mlaji ili aweze kutumia bidhaa zinazokidhi ubora.

Mahilla, anasema baada ya kusainiwa kwa mkataba wa mita leo hii vipimo haviwezi kutofautiana isipokuwa changamoto inaweza kutokea kwa sababu ya nchi kutofautiana vifaa.

Anasema katika vipimo, kuna vipimo vya hali ya juu zaidi, vipimo vya kati na vya chini kulingana na mahitaji ya nchi husika.

Anafafanua huwa wanafanya mlinganyo wa vipimo, mfano linapoletwa jiwe la kilo moja nchini Tanzania, wao kupitia maabara ya ugezi wanalipima linapelekwa Sweden linapimwa na likitoka hapo linazungushwa nchi nyingine baada ya kuwa wamemaliza kulipima wanaanza kuangalia majibu ya kule kote ambayo jiwe hilo limepimwa kama yanalingana.

"Kuna sehemu ambako kipimo chako ili kikubalike lazima kiwe kimefika kati ya ngapi hadi ngapi, kwa hiyo kikiwa ndani ya kile kipimo kilichokubalika, inahesabika vipimo vyako vipo sahihi," anasema Mahilla Mahilla anasema Ugezi umegawanyika katika makundi matatu, nayo ni vipimo vya kisayansi,sayansi ya vipimo viwandani ambayo ndiyo TBS inahusika nayo na vipimo vya kisheria, ambavyo kwa hapa nchini vinakuwa chini ya Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA).;

" WMA vipimo vyao wanaleta kwetu tunawapimia halafu wao wanaenda kuwapimia wateja. Wanavileta kwetu kwa sababu sisi ndio watunzaji wa vipimo vya kitaifa na kupitia maabara hii," anasema.

Hata hivyo, Mahilla anasema wapo watu binafsi wanaojihusisha na upimaji, lakini nao vipimo vyao wanavipeleka kwenye maabara ya Ugezi TBS wanawapima, halafu na wao wanakwenda kupimia wengine.

Mahilla anafafanua kwamba vipimo vya biashara na vya kisheria hivyo vinakuwa chini ya WMA, hivyo wao kama shirika wanachokifanya ni kuwapimia vipimo vyao kuona kama vifaa vyao vina ubora gani, halafu wao wanaenda kupimia wateja.

Anapoulizwa kuhusu umuhimu wa vipimo katika nyanya za afya, kilimo, viwandani, Mahilla anasema vipimo vina muhimu mkubwa kwenye nyanja za usalama kwenye afya au hata kwenye chakula.

Anatolea mfano usalama wa chakula kwa watu wa mahoteli, akisema huwa wana majokofu ambayo huwa yanatunza vyakula na kwenye majokofu hayo kuna hali joto ambapo chakula fulani kinatakiwa kitunzwe katika joto la kiwango fulani.

Eneo lingine ambalo Mahilla analitolea mfano ni kwenye viwanda vya madawa, akisema wanatengeneza iwe ni dawa ya maji au kidonge, wanaanza mchakato wa kutengeneza dawa hizo kwa kutumia vipimo hadi mwisho.

Kwa upande wa usalama wa ubora wa bidhaa, Mahilla anatolea mfano uzalishaji mkate, akisema ili utengeneze mkate kuna kiwango ambacho kinahitajika.

"Kama ni sukari kiasi gani unataka kutumia nacho ni kipimo utapima, maji kiasi gani nacho kinakuwa ni kipimo, lazima ujue uchanganye maji kiasi gani, hivyo ukishapata mchanganyiko itabidi uende kwenye mashine za kuokea, hapo itabidi ujue linahitajika hali joto kiasi gani na kama haisomi vizuri maana yake itafika wakati fulani huo mkate utaungua " anasema.

Kuhusu maeneo ambayo Maabara ya Ugezi (Metrology), imepata cheti cha umahiri (Accreditation) wa utendaji kazi kwa kuzingatia kiwango cha kimataifa cha ISO\IEC17025.

Mahilla anasema ni katika eneo la urefu (Dimensional) jotoridi (Temperature), Tungamo (Mass), Ujazo mdogo (Small Volume).

Vyeti hivyo vya umahiri vilitolewa Shirika la SADCAS (Southern African Development Community Acreditation Services).

Anasema kutokana na maabara hiyo kupewa cheti cha umahiri kuliifanya itambulike duniani kote na kuifanya Tanzania kuwa ya nne barani ya Afrika, ikitanguliwa na nchi za Kenya, Afrika Kusini na Misri.

Vigezo vinavyotumika ili maabara itambuliwe kimataifa ni lazima iwe na mfumo rasmi (ulioandikwa) wa utendaji kazi, umahiri wa utendaji kazi kwa wafanyakazi wenyewe katika ugezi, mbinu zinazotumika katika ugezi ziwe zinakubalika kimataifa.

Vigezo vingine ni mazingira ya upimaji na ugezi kukubalika kimataifa na uwiano wa majibu. Pia upatikanaji wa vielelezo vinavyoonesha mchakato mzima wa upimaji hadi matokeo kupatikana ni jambo la umuhimu.

Anapoulizwa kuhusu matarajio ya maabara hiyo, Mahilla anasema ni kuhakikisha wanapanua wigo wa ufanyaji kazi akisema kuna maeneo ambayo hawana vifaa.

"Kwa hiyo matarajio yetu ni kuhakikisha wanapanua wigo wa vipimo ili tuweze kupima katika maeneo mengi zaidi," anaeleza Mahilla.

Anatoa mfano kwenye mashirika ya ndege akisema kuna maeneo mengi ya vifaa ambayo huwa hawapimi kutokana na kutokuwa na vifaa vya kisasa vya kuweza kuwapimia, hivyo wao wenye mashirika hayo ya ndege huwa vifaa vyao wanapeleka nje na wanapimiwa.

Hata hivyo anasema vifaa vingine vya ndege ambavyo wana uwezo navyo vinapimwa katika maabara ya ugezi.

**Kuhamia jengo jipya**

Kuhusu mpango wa shirika, Mahilla anasema ni kuwa na maabara ya kisasa hasa baada ya kukamilika jengo jipya. Anasema vitu vingi tayari vimehamia kwenye jengo jipya, kuna baadhi bado vipo jengo la zamani, lakini baada ya miezi mitatu watakuwa wamehamia jengo jipya.

Anasema kuna mahitaji maalum katika maeneo ambayo wamepata ithibati, hivyo kuna utaratibu ambao umeandikwa ambao unatakiwa kuutekeleza kabla ya kuanza kuhamia kwenye jengo jipya kutoka lile la zamani.

"Kwa namna hiyo kunakuwa na wateja wengi ambao wanahitaji ithibati, maana yake tukisimamisha haraka haraka wakija kukaguliwa watakutwa vifaa vyao vimepimwa na maabara ambayo haina umahiri," anasema Mahilla na kuongeza;

**Mpango wa kununua vifaa**

Mahilla anasema tangu mwanzo kulikuwa na mpango wa kununua vifaa zaidi kwa ajili ya maabara hiyo, lakini hiyo ilishindikana kwa sababu mwanzoni eneo lilikuwa ni ndogo, lakini sasa wana eneo kubwa zaidi la kuweka vifaa vingi zaidi.

**Wateja kwenda kugezi**

Kuhusu mwitikio wa wenye viwanda kwenda kugezi TBS, Mahilla anasema mwitikio ni mkubwa kwa sababu kuna maeneo mengi wateja wanahitaji. "Manzoni kulikuwa na maeneo ambayo wateja walihitaji kufanyiwa ugezi, lakini sasa wameongezeka zaidi," anasema.

kizungumzia faida za kutumia vipimo sahihi, Mahilla anasema ni kuwa na uhakika na kile unachopima na uhuduma unayotoa. Anatoa mfano kwamba daktari anatoa dawa kwa mgonjwa baada ya kupata vipimo sahihi na vivyo hivyo ndivyo ilivyo viwandani.

Anasema bidhaa ikipimwa na vipimo vilivyo sahihi, maana yake bidhaa inakuwa ni bora na katika maeneo mengine hata kwa wajenzi wa majumba, barabara zitakuwa kwenye ubora zaidi.

**Majukumu ya maabara ya ugezi**

Mahilla anasema majukumu ya maabara ya ugenzi ni utunzaji viwango vya kitaifa. Anasema kuna viwango vya vipimo vya aina mbili.

Anasema vipo ambavyo vipo kwenye makaratasi (maandishi), lakini wao TBS kiwango chao kipo kwenye vifaa. "Kwa hiyo sisi jukumu la kwanza ni kutunza viwango vifaa vya taifa.

Jukumu la pili ni kutoa unasibishaji wa vipimo, kwa sababu sisi ni maabara ya taifa, vipimo vyote tulivyonavyo kwenye maabara ya ugezi, vipo kwenye ubora wa hali ya juu kwani sisi ndio tunapimiwa vifaa vyetu kwenye maabara za kimataifa nje ya nchi na kuvileta kwenye maabara yetu ili kupima vifaa wateja wengine ambao ndiyo watu wa mwisho wa kutumia vipimo."

Anasema jukumu la mwisho ni kupima vifaa vya wateja na watu wengine. Lakini pia anasema wanatoa mafunzo kwa watu mbalimbali kuhusiana na umuhimu wa vipimo na mtu yeyote anayehitaji kujifunza, wanatoa elimu hiyo.

**Athari za kutumia vipimo visivyo sahihi**

Mahilla anataja athari za kukwepa vipimo anasema ni kupata hasara, maana unaweza kuzalisha vifaa vingi na kama havipo kwenye viwango matokeo yake ni kupata hasara.

Anatoa wito kwa watumiaji wa vipimo wawe na vipimo vilivyo sahihi, kwani kudhibiti ubora kunaanzia kwenye vipimo, hivyo ni muhimu wadau mbalimbali kuhakikisha vipimo vyao vipo katika hali iliyo nzuri.

## HABARI KIMATAIFA

# Wamarekani wamuaga George Floyd

**MINNEAPOLIS,** Marekani

TARATIBU za kuaga mwili wa George Floyd, ambaye kifo chake kimesababisha maandamano makubwa nchini kote Marekani, zimeanza rasmi mjini Minneapolis, huku watu mbalimbali maarufu wakitoa wito wa kuendelea na maandamano.

Maelfu ya watu waliokusanyika kutoa heshima zao kuanzia siku ya Alhamisi, walikaa kimya kwa dakika nane na sekunde 46, muda ambao Floyd, anadaiwa alitumia akiwa amekandamizwa shingo yake chini na polisi mzungu kabla ya kufariki dunia.

**Hatutaacha (kuandamana), tutaendelea mpaka tutakapobadili mfumo uwe wa haki.**

Baadhi ya watu mashuhuri walihudhuria tukio hilo, mwanaharakati wa asasi za kiraia Mchungaji Al Sharpton, alitoa ujumbe wake akisema ni wa kusimama na kuondoa mguu kwenye shingo za watu weusi.

Mchungaji Al Sharpton, alitaka uwajibikaji katika nyanja zote hadi mabadiliko yaonekane.

"Hatutaacha (kuandamana), tutaendelea mpaka tutakapobadili mfumo uwe wa haki,' aliwaambia waombolezaji

Video iliyomuonyesha Floyd, akikandamizwa kwa goti na polisi mzungu, Derek Chauvin, imeibua wimbi la maandamano katika miji mbalimbali nchini Marekani.

Chauvin na polisi wengine wawili Tou Thao, J. Alexander Kueng, na Thomas Lane, wamefikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza. Washtakiwa walitakiwa kulipa dola milioni moja kama dhamana, lakini itapunguzwa hadi dola 750,000 ikiwa watasalimisha silaha zote wanazomiliki.

Akizungumza katika utoaji heshima, Benjamin Crump, ambaye ni wakili alisema si 'janga' la corona lililomuua Floyd, bali ni ubaguzi wa rangi.

Gavana wa Minnesota, Tim Walz, Seneta wa Minnesota Amy Klobuchar na Meya wa Minneapolis, Jacob Frey, ni miongoni mwa watu waliohudhuria katika tukio hilo lililofanyika katika Chuo Kikuu cha North Central mjini Minneapolis.

Mmoja wa ndugu wa Floyd, Philonise Floyd, alieleza jinsi familia ilivyoishi kwenye umasikini na namna George, alivyokuwa akijitahidi kukabiliana na hali hiyo, kiasi cha kufua nguo zake na kuzikausha kwa kutumia mashine ya kupashia joto chakula.

"Watu wote hawa wamekuja kumuona kaka yangu, inashangaza aligusa mioyo ya watu wengi sana," alisema. **BBC**



Waombolezaji wakisukuma jeneza la marehemu George Floyd kuingia katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha North Central mjini Minneapolis kwa ajili ya ibada ya kuaga mwili wake. **PICHA: AFP**

## UN wazindua mpango mpya wa mazingira

**NEW YORK,** Marekani

UMOJA wa Mataifa umezindua mpango mpya katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mpango huo umezinduliwa jana katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, yakiwa na kauli mbiu "kuikimbilia sifuri" lengo ni kusitisha utoaji wa gesi chafu kufikia mwaka 2050.



Karibu kampuni 1000, miji 458, majimbo na kanda 24, vyuo vikuu 500 na wawekezaji 36, wamekubali mpango huo wa kusitisha utoaji wa gesi chafu.

Miongoni mwa kampuni kubwa zilizokubali ni kampuni ya magari ya Rolls Royce na Nestle.

Zaidi ya nchi 120 pia zimetoa ahadi hiyo. Rais wa mkutano mkuu ujao wa mazingira, Alok Sharma (pichani), alisema mpango huo unataka kuzifanya kampuni na serikali kudhamiria kuhifadhi mazingira. **DW**

## Chloroquine yawahangaisha WHO

**ZURICH,** Uswizi

UTAFITI mpya umebaini kulikuwa na hila ambayo imechangia kuahirishwa kwa majaribio ya dawa ya hydroxychloroquine, kutibu ugonjwa wa Covid 19.

Katika majaribio ya awali, ilionekana dawa hizo zinaongeza hatari ya kifo kwa wagonjwa wa virusi vya corona na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuamua kuahirisha kutokana na kuwapo kwa maswali yaliyokosa majibu kuhusu data.

Utafiti huu mpya, waandishi wamesema hawawezi tena kuthibitisha ukweli wa matokeo hayo, baada ya kampuni ya masuala ya afya ya Surgisphere, ambayo ilitoa data hizo , kukataa kupitiwa upya kwa kutumia chombo binafsi.

Dawa hiyo ya kutibu Malaria imekuwa ikitumiwa na Rais wa Marekani, Donald Trump, kama njia ya kujikinga na corona kuisifia kuwa inafanya kazi vizuri.

Mkurugenzi mtendaji wa Surgisphere, Sapan Desai, mmoja kati ya watafiti ameliambia gazeti la Guardian, kuwa atatoa ushirikiano na chombo hicho binafsi, lakini kutoa data kunaweza kukiuka makubaliano ya wateja na matakwa ya kuwatunzia siri.

Utafiti wa awali ambao ulichapishwa mwezi Mei kwenye jarida la kitabibu la Lancet , ulihusisha wagonjwa 96,000 wa virusi vya corona katika hospitali 671 duniani. Wagonjwa 15,000 walipewa dawa ya Hydroxychloroquine au inayofanana na chloroquine,

Utafiti huo ulihitimisha kuwa dawa haikuonyesha matunda katika kupambana na virusi vya corona, isipokuwa iliongeza hatari kwa wagonjwa kupata matatizo ya moyo na kusababisha kifo.

Hata hivyo, Profesa Mandeep Mehra, kutoka Chuo cha Havard, Frank Ruschitzka kutoka Chuo cha hospitali ya Zurich na Amit Patel wa Chuo Kikuu cha Utah, walisema wamejaribu kuomba data hizo kupitiwa upya, lakini Surgisphere ilikataa kutoa ushirikiano.

"Tunaomba radhi kwenu, wahariri na wasomaji kwa usumbufu ambao umejitokeza," lilisema jopo hilo.

Kumekuwa na maoni mbalimbali ya wanasayansi kuhusu matumizi ya dawa hiyo katika kutibu virusi vya corona.

Hydroxychloroquine ni salama kwa kutibu malaria, na maradhi mengine kama vile lupus na baridi yabisi, lakini mpaka sasa hakuna majaribio yaliyokubalika kuwa inaweza kutumika kama tiba ya Covid-19.

Matokeo ya majaribio katika Chuo cha Minnesota, yalionyesha kuwa hydroxychloroquine, haina ufanisi wa kuzuia virusi vya corona.

Wakati huo huo, WHO katika taarifa yake iliyotolewa Juni 3 mwaka huu, ilisema itaendelea na majaribio yake baada ya kuahirishwa mwezi uliopita.

Mwezi Machi, Shirika la Dawa na Chakula nchini Marekani liliidhinisha matumizi ya dharura ya dawa hiyo, lakini matumizi hayo yaliruhusiwa kwa wagonjwa wachache waliolazwa.

Kiongozi mwingine anayeipigia chapuo dawa hiyo ni Rais wa Brazil, Jair Bolsonari, ambaye alidai kuwa Hydroxychloroquine inafanya kazi vizuri katika maeneo yote. **BBC**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa wa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini- **17**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

HAPO ndipo Eddy alipojigundua kuwa, kile kitu ambacho anakiona hakipo sawa kwake, ni kutaka kumuona tena Shani kwa mara nyingine.

“Ndiyo. Nahitaji kumuona.” Alijiambia. “Lakini siyo sasa. Kwa sasa ndiyo kwanza ametoka kwenye arobaini ya baba yake. Subiri kwanza atulie. Lakini lengo ni nini?” Alijiuliza.

“Hakuna lengo maalum. Huyu kwanza anaweza kunipa mambo mengi juu ya marehemu baba yake, pamoja na shangazi yangu na katika maongezi anaweza kusema jambo ambalo linaweza kuanzisha upelelezi wa mauji yaliyotokea harusini kati ya baba yake na shangazi yangu.” Alijijibu mwenyewe.

Tangu alipokuwa Marekani alijiapiza kuwa kazi yake ya kwanza atakaporejea ni kuomba wakubwa wake wa kazi wampe faili na kibali cha kupeleleza na kuchunguza vifo hivyo ambavyo viliitemesha si Tanzania tu, bali hata dunia nzima.

Ingawa alifanya kazi kubwa huko nyuma na kupata umaarufu mkubwa kutoka kwa mabosi wake, lakini kwa muda wa mwaka mmoja wa masomo, atataka kuwathibitishia mabosi wake kuwa kwa sasa ameiva zaidi tofauti ya ilivyokuwa awali.

Kwanza kabisa ni kutaka kuthibitisha ubora wake na masomo yake yalikuwa ya hali ya juu, lakini pia kulipa kisasi cha kuuawa shangazi wake.

“Nadhani na kuuawa kwa baba yake Shani pia. Atanishukuru sana. Na yeye nadhani atarejewa na furaha kama wasichana wengine.” Alijisemea mwenyewe na usingizi mzito ukampitia hapo hapo kwenye kochi.

**************************

“Una uhakika kuwa kazi hiyo unaiweza bila kuleta mushkeli wowote ule?” Muulizaji aliuliza huku macho yake yakionyesha wasiwasi.


“Nimekwambia hiyo ni kazi ndogo tu. Si kuweka sumu kwenye kinywaji au chakula chake tu basi, au kuna kingine?”

“Ni hicho tu.”

“Basi hakuna tabu, mimi nipe milioni mbili nikufanyie kazi, maana kazi ya kuua mtu si masihara, basi tu njaa zetu hizi.”

Ilikuwa kwenye mgahawa mmoja maeneo ya Kariakoo, Jim alikuwa amekutana na mmoja wa wafanyakazi wa hoteli ya ABC Club, maeneo ya Mbezi Beach.

Jim ambaye kwa sasa ana miaka 65, ndiye aliyebeba dhamana yote




**Ilikuwa kwenye mgahawa mmoja maeneo ya Kariakoo, Jim alikuwa amekutana na mmoja wa wafanyakazi wa hoteli ya ABC Club, maeneo ya Mbezi Beach.**

ya ndugu zake watatu, George, Paul na Ben ambao wote ni wadogo wake kiumri.

Wazo lao ni kutaka kukomba mali zote za marehemu ndugu yao wa baba na mama mmoja kwa kuzaliwa, Patiyo, milionea aliyeuawa wakati anatoka kufunga ndoa kanisani na mkewe Grace Maumba.

Kikwazo pekee ni binti wa pekee wa marehemu Shani, msichana mbichi, msomi mwenye umri wa miaka 23 tu, ambaye taratibu zote wa kisheria za kurithi mali na makampuni ya baba yake alikuwa yamekamilika.

Kilichobaki ni siku na saa tu ya kukabidhiwa nyaraka, kitu ambacho Jim na ndugu zake walikuwa hawataki hata kusikia.

“Kwanza tuna nusu mzigo hapa. Milioni moja hii hapa keshi na ukishamaliza kazi, tunamalizia pesa iliyobaki.” Jim alisema, mkononi akiwa na bahasha ya rangi ya khaki, akikabidhi kijana mwenye umri usiozidi miaka 26 hivi.

Jina lake ni Fikiri. Alizaliwa Kilwa na alichukuliwa na mjomba wake kwenda Dar baada ya kumaliza darasa la saba na kushindwa kuendelea mbele na masomo.

Akiwa Dar, kwa bahati nzuri hakuchagua kazi. Aliweza kufanya kazi yoyote iliyomuingizia kipato.

Uchangamfu wake uliweza kumfanya kujuana na kukutana na watu wengi. Mmoja wapo ndiye alikuwa amepata kazi kwenye hoteli ya ABC Club, naye alipoambiwa amtafute mtu mwingine kama mhudumu wa kiume, alimfuata rafiki yake Fikiri na kumuunganisha.

Mishahara alioupata ulimtosha kuishi maisha ya kawiada ya yaliyokuwa ya kubabaisha.

Tatizo kubwa la Fikiri ilikuwa ni kupenda sana wanawake. Tayari alikuwa wameshazaa na wanawake watatu tofauti, ingawa bado hajaona mpaka sasa.

Wanawake wote hao walihitaji matunzo ya watoto wao, lakini pia mwenyewe akihitaji pesa za kujirusha na wasichana wengine.

Kutokana na hali hiyo pesa haikutosha kabisa. Ndiyo maana ulipokuja mpango huo wa kuweka sumu kwenye chakula au kinywaji cha Shani, alikubali.

Pamoja na kujua kuwa anaweza kujikuta hatiani, lakini pia alijua akifanikiwa atakuwa ametatua matatizo yake kwa kiasi kukubwa.

“Milioni mbili siyo mchezo. Sijawahi kuzipata tangu nizaliwe.” Alijisemea moyoni alipofuatwa na Jim kuhusu mpango huo.

Awali alikuwa na hofu. Lakini alipoambiwa kuwa anachopewa ni sumu baridi. Sumu ambayo itamuua mtu baada ya miezi mitatu au minne.

Ni siku nyingi sana kwa sababu, binadamu atakuwa amepitia sehemu mbalimbali, hivyo si rahisi sana kwa polisi kuchunguza na kugundua kuwa aliipatia wapi.

Aina ya sumu aliyopewa, aliambiwa kuwa inafanya kazi ya kumfanya aliyepewa kugunduliwa na ugonjwa wa kansa, atakapofanyiwa uchunguzi.

Hilo ndilo lilimfanya aingie kwenye dili hilo chafu la kutaka kumuwekea sumu msichana mrembo Shani.

*************************

Alisikia simu yake ikiiita. Alichukua na kuangania jina. Moyo ulimshtuka kwa mbali.

“Shani.” Alitamka na mwenyewe hakujua kama alikuwa akisema au kuuliza.

“Halo mrembo vipi mambo?” Haraka haraka alianza kumuuliza, kabla hajasalimiwa.

Alijiona kama vile nafsi inamsuta. Ni yeye ndiye aliyepigiwa simu badala ya yeye kupiga.

Hata hivyo alijipa moyo na kujiambia “Haiwezekani nionekane nimekuwa dhaifu na binti mdogo kama huyu.”

“Hata kunitafuta ndugu yangu?” Sauti ya Shani ilisikika upande wa pili.

“Hapana, unajua nisingeweza kukutafuta haraka haraka tu, nilitaka nikutafute wakati nimetulia na wewe pia umetulia.” Alijibu na kutabasamu, kwani aliona jibu hilo ni muafaka.

“Kweli eee?”

“Ni kweli binamu yangu.”

Eddy alisikia kicheko kikali kutoka kwa Shani.

“Mbona umefurahi sana?”

“Nimefurahi kusikia unanita binamu yangu.”

“Kwani uongo? Baba yako mzazi Patiyo si alimuoa shangazi yangu, sasa kwa nini usiwe binamu yangu?”

“Binamu gani? Au binamu kinyama cha hamu.”

“Vyovyote vile.”

Jibu hilo la Eddy lilimfanya Shani kuangua kicheko kikali kuliko cha mwanzo.

“Binamu leo umeamka na vicheko, tofauti na siku ile kule makaburini.”

“Unanifurahisha, kumbe una maneno hivyo. Wala sikujua hilo.” Shani alisema huku akikohoa kikohozi chepesi

“Nataka siku uje nyumbani hapa, naona kutachangamka kweli, maana kwa muda mfupi tu nimegundua kuwa wewe ni mchangamfu sana.”

“Unafikiri mchamgamfu basi, sema basi tu. Ila hilo la kuja nyumbani kwako naliafiki kwa sababu nataka kuja kukuona ukiwa nyumbani. Nikuone ukipika.”

Bado Shani alikauka na kucheka.

“Unataka ukija nikupikie nini?”

“Ugali, dagaa na mchicha.”

Jibu hilo pia lilikuwa kama kichekesho kwa Shani.

Kwa mbali Shani alianza kuamini kile kitu ambacho alichokuwa akiwaza usiku kucha.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Dastan Wilhem Mlaki** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA Allione yenye namba ya usajili **TCLX 946** yenye chasis namba **T2450021474** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **MAN/HAN/RB/328706/2020**

115764002

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAHAKAMA YA MWANZO KIZUMBI SHINYANGA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**Usimamizi wa Mirathi ya No 17/2020**

**Mnamo leo 12.05.2020**

**Bwana/Bibi: 1. Sarah Paul Ng'wani 2. John Paul Ng'wani 3. Rachel Paul Ng'wani Ameteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Paul Zunzu Ngw'ani**

Aliyefariki mnamo tarehe 16.03.2020 Akiwa ameahidi kusimamia mirathi kwa wema na uaminifu Mirathi isimamiwe kwa kufuata nakala ya wosia wa marehemu uliyoambatanishwa

Muhuri wa Mahakama

Sahihi ya Hakimu na Muhuri wake

Wasimamizi wanauarifu Umma kuwa madeni yote ya marehemu mzee Paul Zunzu Ng'wani yawasilishwe kwenye akaunti No 0152496479700 CRDB Benki kwa majina ya Sarah & Rachel na si vinginenyo

115764202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KELVIN MUTATINA NJUWA** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 448 DDN** aina yake **TOYOTA NOAH** yenye chasis namba **SR400113828.** Kwa yeyote atakeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/430882/2020.**

115764802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NOVROZ IQBAL MURJI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA PICNIC** yenye namba za usajili **T 445 CVX** chassis namba **JTEGH23B300009531** engine namba **1AZ1298744.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IR/IR/RB/799/2020.**

115764702

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;142/2020**

**Ombi la NEEMA ANDERSON NA LOYCE KIMWAGA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PHILEMON DANIEL MAKALA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/06/2020.

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115764902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GREYSON DAMIAN NYANTAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 297 CBV TOYOTA CRESTA.** Engine namba **IG0021052**. Chassis namba **GX1000017392.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/221047/2020.**

115764602


**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BALE HATAKI KUONDOKA MADRID




**MADRID,** Hispania

WAKALA wa mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale, amesema mchezaji wake anataka aendelee kubakia klabuni hapo, na hahitaji kurudi EPL.

Bale amekua anahusishwa na mpango wa kurejea katika Ligi Kuu England, huku klabu yake ya zamani Tottenham Hotspur na Manchester United zikitajwa kumwania.

Winga huyo raia wa Wales mwenye umri wa miaka 30 siku za hivi karibuni alikuwa anahusishwa kurudi EPL baada ya kutokuwa kwenye maelewano mazuri na kocha wake, Zinedine Zidane.

Akizungumzia kuhusiana na tetesi hizo amesema: "Sifikirii kama hilo linaweza kutokea kipindi hiki, licha ya kushindwa karibia kila timu, bado anaonekana kuwa na furaha hapa Madrid," alisema Jonathan Barnett, wakala wa Bale.

"Kurudi EPL itakuwa ni jambo kubwa kwa sababu ya aina ya maisha anayoishi hapa, Hana tamaa ya fedha kama wengine hivyo sioni kama hilo linaweza kutokea".

Tangu ajiunge na Real Madrid kwa rekodi ya aina yake mwaka 2013, Bale ameshinda mataji kama Ligi ya Mabingwa mara nne, La Liga, Copa del Rey, Kombe la Dunia ngazi ya vilabu, na Kombe la Ligi ya Hispania yote mara moja, na Uefa Super mara tatu.

# Moyes alimkataa Pogba kutua Utd

**MANCHESTER,** England

KOCHA David Moyes alipiga chini nafasi ya kumrudisha Paul Pogba ndani ya kikosi cha Manchester United wakati alipochukua mikoba ya kuinoa timu hiyo mwaka 2013.

Moyes alitua Old Trafford kuchukua mikoba ya Sir Alex Ferguson wakati alipong'atuka, lakini alijikuta akidumu kwenye kikosi hicho kwa miezi minane tu kabla ya kupigwa kibuti.

Usajili wa ovyo kwenye dirisha la majira ya kiangazi la mwaka huo wa 2013, ulimshuhudia Moyes akimsajili Marouane Fellaini na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye kufeli kwake.

United ilihitaji kumsajili Pogba kipindi hicho, lakini kiungo wa Hispania, Cesc Fabregas alikuwa chaguo la kwanza la Moyes hivyo alimtaka Makamu Mwenyekiti Mtendaji, Ed Woodward kukatiza likizo yake na kwenda kukamilisha usajili wa staa huyo, ambaye kipindi hicho alikuwa Barcelona.

Lakini, dili lilishindwa kukamilika na miezi 12 baadaye, Fabregas alikwenda kujiunga na Chelsea na kubeba taji la Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza tu tangu atue Stamford Bridge.

Pogba aliondoka United mwaka 2012 kwenda Juventus baada ya kushindwa kupata nafasi kwenye kikosi chini ya Ferguson, lakini miaka minne baadaye, United ikinolewa na Jose Mourinho, staa huyo wa Ufaransa alirudi kujiunga na mabingwa hao mara 20 wa England kwa ada ya pauni milioni 89.




PREMIER LEAGUE

# *EPL yaruhusiwa mabadiliko ya wachezaji watano*

**LONDON,** England

LIGI Kuu England imeruhusu matumizi ya wachezaji watano wa akiba mchezoni badala ya watatu kama ilivyo kwa sasa, ili kutoa nafasi kwa makocha kuwapa mapumziko wachezaji.

Mabadiliko hayo yatatumika katika kipindi hiki cha mpito cha janga la virusi vya corona kwa sababu timu hazijapata muda wa kujiandaa vizuri baada ya ligi kusimama kwa takribani miezi mitatu huku ikitegemewa kuwa na mechi nyingi za karibu karibu.

Makubaliano hayo yamefikiwa na vilabu vyote vya EPL kupitia kikao kilichofanyika leo Alhamisi.

Aidha, kila timu itakuwa na wachezaji tisa wa akiba tofauti na mwanzo ambapo kila timu ilitakiwa kuwa na wachezaji saba pekee wa akiba.

Bodi ya kimataifa inayotunga sheria za kandanda sheria - IFAB walipendekeza kuwapo kwa ongezeko la mabadiliko ya wachezaji mpaka watano katika mashindano tofauti tofauti yaliyo rasmi ili vilabu vipitishe hasa kwa kipindi hiki cha ligi kilichosalia.

Ligi Kuu England itarudi tena Juni 17 huku mechi kubwa ikiwa ni Manchester City dhidi ya Arsenal mchezo wa kiporo kabla ya ratiba ya kawaida kuendelea Juni 19.

# ARSENAL WATAJIWA BEI YA OSIMHEN



**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imetakiwa kulipa pauni milioni 72 kama inataka huduma ya Victor Osimhen kutoka Lille ya Ufaransa.

Osimhen amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mabao 18 kwenye Ligue 1 huku jambo hilo likimfanya awe kwenye rada za klabu kibao za vigogo wakiwamo Washika Bunduki hao wa London.

Kuna timu nyingine kibao zinamtaka mshambuliaji huyo, hivyo Arsenal wameambiwa kama wanamhitaji basi wafanye haraka kabla ya mambo hayajawa magumu kwao.

Nyota huyo wa kimataifa wa Nigeria amekuwa na msimu mzuri huko Ufaransa ambako alitua mwaka jana akitokea kwenye klabu ya Ubelgiji ya Sporting Charleroi kwa ada ya pauni milioni 10 kwenda kuziba pengo la Pepe.

Na Arsenal sasa wanataka kurudi huko Lille kwenda kumsajili Osimhen, lakini walichoambiwa ni kwamba wanapaswa kulipa kiwango kama walicholipa kwenye usajili wa Pepe.

Mmiliki wa klabu hiyo, Gerard Lopez alisema: "Kuna ofa kadhaa ziliIetwa. Tulikataa moja kutoka England na nyingine kutoka Hispania kwenye dirisha la Januari. Kuna ofa nyingi zaidi kwenye dirisha hili la majira ya kiangazi, lakini sitaki kutaja majina ya timu zilizoleta ofa hizo."

## Corona yaikumba Spurs

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imethibitisha taarifa za mfanyakazi wake mmoja kubainika ameambukizwa virusi vya corona.

Mfanyakazi huyo amethibitika kuwa na virusi hivyo katika kundi la watu 1,197 waliofanyiwa vipimo wiki hii.

Hata hivyo, klabu hiyo ya Kaskazini mwa jiji la London haijaweka hadharani jina la mfanyakazi huyo kutokana na sheria za kitabibu. Katika taarifa yake iliyotolewa jana, Tottenham ilisema kuwa tayari mhusika ameshaanza kuchukua hatua stahiki baada ya kubainika kuambukizwa virusi hivyo.

"Kwa sasa hana dalili zozote lakini atatakiwa kujitenga na kukaa mwenyewe kwa siku saba kuendana na protokali ya Ligi Kuu England.

"Tutaendelea kuchukua tahadhari na kufuata protokali ya kurejea mazoezini ambayo ni ya kuhakikisha uwanja wetu wa mazoezi unabakia kuwa salama na mazingira huru dhidi ya virusi vya corona," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa kanuni za afya zilizopitishwa na serikali ya Uingereza katika kipindi hiki cha corona, iwapo aliyeathirika angekuwa ni mchezaji, mechi za Tottenham zingelazimika kusogezwa mbele.

Ligi Kuu England inatarajiwa kurejea Juni 17, mwaka huu ambapo kutakuwa na mechi mbili. Mechi moja itakuwa ni baina ya Arsenal na Manchester City na nyingine itakuwa baina ya Aston Villa na Sheffield United.





## Liver wapewa muda kwa Werner

**MUNICH,** Ujerumani

LIVERPOOL na Chelsea zimeelezwa kwamba zimebaki na siku zisizozidi 12 kukitumia kipengele kilichopo kwenye mkataba wa Timo Werner kinachosema mchezaji huyo anaweza kupatikana kwa pauni milioni 49.

Siku hizo zitakapopita, klabu yake ya RB Leipzig itakuwa na nguvu ya kupanga bei wanayotaka kumuuza mshambuliaji huyo ambaye amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu.

Klabu kadhaa hasa za Ligi Kuu England zimevutiwa na ubora wa Werner anaoonyesha huko kwenye Bundesliga na hivyo wanachuana kwa nguvu zote kumfukuzia.

Kipengele hicho kinachotaja kwamba Werner anapatikana kwa pauni milioni 49 kitafika mwisho wake Juni 15 na baada ya hapo, suala la kunasa huduma yake litakuwa gumu kwa sababu RB Leipzig watakuwa na uamuzi wa kumuuza au kuacha huku wakipata nguvu pia ya kupanga bei wanayotaka.

Liverpool wanatajwa kuwa mstari wa mbele kwenye kumfukuzia mshambuliaji huyo huku Chelsea nao wakiibuka siku za karibuni kwamba wanahitaji aende akaboreshe safu yao ya ushambuliaji.

Mkataba wa Werner kwenye kikosi cha RB Leipzig utafika tamati majira ya kiangazi mwaka 2023, lakini kipengele kilichokuwa kimewekwa kwenye mkataba wake kilikuwa kinamruhusu kuondoka mapema zaidi kabla ya muda huo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAJIPANGA KUMSAJILI CHILWELL

Beki huyo amekuwa chaguo la muda mrefu la Lampard, ambaye amedhamiria kufanya...

**LONDON,** England

BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell (23), anahusishwa na mpango wa kujiunga na Chelsea katika kipindi cha majira ya joto lakini bado hajaweka wazi rasmi kama anataka kuondoka Leicester City.

**Chilwell anajiandaa kujiunga na Frank Lampard katika mpango wake wa kufanya mapinduzi kwenye kikosi cha Chelsea ifikapo majira ya joto, linaandika gazeti la The Mirror.**

Beki huyo wa kushoto amekuwa ni chaguo la kwanza la Lampard ambaye amekuwa akivutiwa naye kwa muda mrefu na anamatumaini ifikapo majira ya joto mchakato huyo wa kutua Stamford Bridge utakamilika.

Hata hivyo, The Foxes imesema thamani ya Chilwell iko juu kuliko ilivyomuuza Harry Maguire, ambaye alinunuliwa na Manchester United kwa dau la pauni milioni 80 majira ya joto mwaka jana.

The Mirror liliendelea kuandika kuwa Chilwell bado hajaniambia chochote Leicester kama anataka kuondoka, huku kikosi hicho kinachoongozwa na Brendan Rodgers kikipambana kusaka tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Leicester inataka kulipwa zaidi ya pauni milioni 85 ili kumuuza mchezaji huyo ambaye alikulia kwenye akademi yao, ingawa taarifa zinadai Chelsea inaamini itapata chini ya kiasi cha fedha kwa sababu ya klabu kuyumba kiuchumi kutokana na janga la ugonjwa wa corona.

Kama Rodgers atafanikiwa kumaliza kwenye nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England msimu huu, kwa sasa Leicester iko kwenye nafasi ya tatu, pointi tano zaidi ya Chelsea, hiyo itaipa nguvu ya kumbakisha Chilwell klabuni hapo kwa msimu mwingine.

Beki wa kushoto wa Arsenal, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 23, anatajwa huenda akawa mrithi sahihi baada ya kuwa na wakati mgumu katika msimu wake wa kwanza ndani ya Emirates.

Rodgers aliwahi kufanya kazi na nyota huyo raia wa Scotland katika kikosi cha Celtic, lakini anadai kwamba anataka kuendelea kubakia hapo na kumthibitishia Kocha wa Gunners, Mikel Arteta kwamba anaweza kupata namba katika kwenye kikosi chake cha kwanza.

Majeruhi ya mara kwa mara yalimfanya Tierney kushindwa kufanya vema kama alivyotarajiwa na akakiri anataka kuhama katika klabu hiyo ya London Kusini na kwenda kujaribu maisha kwenye jiji lingine.

Wakati huo huo, Chelsea imeizidi nguvu Liverpool katika mchakato wa kumsajili straika wa RB Leipzig, Timo Werner. Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani amesaini mkataba wa miaka mitano na atalipwa mshahara wa pauni 180,000 kwa wiki baada ya Blues kukubali kulipa ada ya pauni milioni 53.

## ZISIKUPITE

### VERTONGHEN MTEGONI

MABOSI wa Tottenham Hotspur wanasubiri kuona kama beki wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen (33), ataamua kuondoka sasa au atasubiri mpaka msimu huu utakapofikia ukingoni. ***(Sky Sports)***

### LONGSTAFF ATAKIWA ITALIA

KIUNGO wa Newcastle United, Matty Longstaff (20), hajafanya mazoezi kwa sababu ya kutojua hatima yake ndani ya klabu hiyo, huku tayari amepokea ofa ya kujiunga na timu ya Serie A, Udinese ambayo imepanga kumlipa mshahara wa pauni 30,000 kwa wiki. Nyota huyo raia wa England anatarajia kumaliza mkataba wake majira ya joto. ***(Mail)***

### CITY, GARCIA KUTETA

MANCHESTER City inajipanga kufanya mazungumzo ya kusaini mkataba na beki wake Mhispania Eric Garcia (19), ambaye anatajwa kuwindwa na klabu yake ya zamani ya Barcelona. ***(Mail)***

### WILLIAMS MAMBO SAFI

MANCHESTER United inajiandaa kumpa mkataba mpya beki wake, Brandon Williams (19), ambao utakuwa na mshahara mpya wa pauni 40,000 kwa wiki baada ya kuonyesha kiwango kizuri msimu huu. ***(The Athletic - subscription required)***

### LIVERPOOL YAJIWEKA TAYARI

LIVERPOOL inatarajia kutangaza ubingwa wake wa Ligi Kuu England Jumapili usiku wakati ikiikabili Everton, ambao ni mchezo wa pili baada ya ligi hiyo kurejea na michezo yote ikipangwa kufanyika jioni. ***(Mail)***

### TIERNEY AWEKWA SOKONI

ARSENAL inaangalia uwezekano wa kumuuza beki wa Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney (23), kwa Leicester City, ikiwa ni miezi 12 imepita tangu nyota huyo atue katika klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Emirates. ***(Express)***

### GRIEZMANN AFUNGUKA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann ambaye ana umri wa miaka 29, ameweka wazi kuwa anapenda kustaafia soka katika Ligi Kuu Marekani. ***(LA Times)***

### RAKITIC HANA HARAKA

KIUNGO wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (32), atajadili mchakato wa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Sevilla itakapofika mwisho wa msimu. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### RABIOT AWEKA MGOMO

KIUNGO wa Juventus, Adrien Rabiot (25), anatajwa kuwindwa na Everton na Arsenal, lakini Mfaransa huyo bado hajakubali kuona mshahara wake unapunguzwa endapo ataondoka katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Tuttomercato - in Italian)***

### HAVERTZ NJIA PANDA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz, ambaye anawindwa na Real Madrid, Mkurugenzi wa Michezo wa Bayer Leverkusen, Simon Rolfes amesema bado klabu hiyo ya Bundesliga haijafanya uamuzi kuhusiana na hatima ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Marca)***

## Azam yamnyima ‘usingizi’ Wawa

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI wa kati wa kimataifa wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Pascal Wawa, amekiri mchezo wa robo fainali wa Kombe la FA dhidi ya Azam FC utakuwa mgumu kutokana na ubora wa vikosi vya timu hizo mbili.

Akizungumza na gazeti hili, Wawa alisema wachezaji wa Simba hawana wasiwasi na mchezo huo na wamejipanga kuendeleza ushindi dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Kombe la FA.

Wawa alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu tayari waliwafunga Azam katika mchezo uliopita wa Ligi Kuu Bara, lakini pia wapinzani wao wakitegemea tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa kupitia kombe hilo.

“Azam ni timu nzuri tunaijua, kila tunapokutana basi mechi huwa ngumu, ushindani pia unakuwa mkubwa lakini tutajipanga kuhakikisha tunapata matokeo ya ushindi na kusonga mbele,” alisema beki huyo wa zamani wa Azam na El Merreikh ya Sudan.

Wawa alisema sababu ya kujiamini watapata matokeo mazuri ni uzoefu wa wachezaji wa kikosi cha Simba.

“Kwa upande wangu ninafanya mazoezi kwa bidii, ninajua washambuliaji wengi wanaocheza Ligi Kuu ni wazuri na wanafanya vizuri katika nafasi zao, wamekuwa wakimsumbua lakini hawapiti kirahisi.” alimaliza.

## Ligi Kuu Z’bar kuchezwa Unguja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema Ligi Kuu Zanzibar ambayo inashirikisha timu 16 sasa itachezwa katika kituo kimoja cha Unguja, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu wa ZFF, Ali Ameir, alisema ligi hiyo itachezwa kwenye viwanja vitatu ambavyo ni pamoja na Mau A, Mau B na Amaan.

Ameir alisema uamuzi wa kucheza ligi hiyo katika kimoja umetokana na kutaka kuziepusha timu kusafiri na kupambana na maambukizo ya virusi vya corona.

“Usafiri wa visiwa vya Zanzibar kutoka Unguja kwenda Pemba na kurudi mara nyingi tunatumia meli, na kama tunavyojua timu zinapaswa kusafiri mara nyingi kutokana na idadi ya michezo iliyopo, Wizara ya Michezo na Wizara ya Afya zimeona ni vema ichezwe katika kituo kimoja ambapo wachezaji wote watawekwa kambini na hawatasafiri,” alisema Ameir.

Hata hivyo alisema mechi za awali zitachezwa bila ya mashabiki mpaka pale serikali itakaporuhusu baada ya kuangalia hali ya ugonjwa wa corona itakavyokuwa.

Alisema pia kuanzia jana, timu zote zimeruhusiwa kufanya mazoezi ya pamoja huku zikisubiri ratiba itakayotolewa na Bodi ya Ligi Zanzibar.

# NAMUNGO FC YAJIPANGA KUZIBANA SIMBA, YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana amesema malengo ya timu yake ni kucheza fainali ya mashindano ya Kombe la FA, hivyo wamewatahadharisha Alliance FC kujiandaa kupokea kichapo katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema wanaendelea vema na maandalizi ya mchezo huo pamoja na mingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia.

Hitimana alisema ameanza kuwapa mbinu mpya wachezaji wake kwa ajili ya kuhakikisha viwango vyao vinaimarika na kuwa tayari kukabiliana na ushindani wowote.

**Kocha huyo alisema anahitaji kuweka historia nzuri kwake ikiwamo kumaliza msimu wa Ligi Kuu Bara katika nafasi tano za juu huku pia akitamani kutwaa ubingwa wa taji la Kombe la FA.**

“Sitaweza kuweka historia hiyo bila ya ushirikiano mzuri kutoka kwa vijana wangu, nimezungumza nao na kila mmoja wao anahitaji kucheza fainali, hivyo inatulazimu kumfunga Alliance ili tucheze tusonge mbele,” alisema Hitimana.

“Tunawaheshimu wapinzani wetu ambao tutacheza nao katika hatua ya robo fainali, tumeshakutana nao katika ligi na kutoka nao sare, sasa tunajiandaa kupata ushindi katika mchezo huo wa mtoano,” Hitimana alisema. Aliongeza wachezaji wake wana morali nzuri na wameahidi kuleta mapinduzi kwenye Ligi Kuu Bara pamoja na michuano ya Kombe la FA ambayo hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho.



Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete (kulia), akiteta jambo na Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, katika sherehe za utiaji saini wa mkataba wa kuelekea katika mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa klabu hiyo na LaLiga.
**PICHA: MTANDAO**

# Ndanda FC yasaka Sh. milioni 73

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WADAU mbalimbali wa soka zikiwamo halmashauri tisa za mkoa wa Mtwara wameombwa kuchanga kiasi cha Sh. milioni 73 ili kuisaidia timu ya Ndanda FC iweze kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, wakati alipokuwa akifunga kikao cha Baraza la Halmashauri ya Mji Masasi cha kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za halmashauri hiyo.

Byakanwa alisema uongozi wa Ndanda unakabiliwa na changamoto ya kifedha na ili kuinusuru na janga la kushuka daraja, wanahitaji kupata kiasi hicho cha fedha ili kuihudumia timu hiyo.

Alisema uendeshaji wa timu hiyo umekuwa ni mgumu kwa sababu hadi sasa wanadeni la Sh. milioni 48 ambazo wanatakiwa kulipia posho za wachezaji na kugharamia usafiri wa mechi zilizosalia za ligi.

“Hali ya kifedha ya timu ni tete, zinahitajika jumla ya Sh. milioni 73, bila wadau kuchangia, timu hiyo itakuwa katika wakati mgumu wa mechi zake zilizobakia ikiwamo kushindwa kulipa posho za wachezaji wake,” alisema Byakanwa.

Kiongozi huyo ambaye ni mlezi wa timu anaomba wadau mbalimbali wa mkoa huo kujitokeza kuichangia Ndanda ili iweze kufanya vizuri na hatimaye kusalia kwenye Ligi Kuu na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA.

“Naziomba halmashauri zote tisa za mkoa wangu kuichangia Ndanda ili kufanikisha upatikanaji wa fedha hizi ambazo zitaiwezesha timu yetu kufanya vizuri zaidi, mkakati uliopo ni Ndanda kubakia katika Ligi Kuu na sio kushuka,”alisema Byakanwa

Aliwaagiza wakuu wa wilaya wote mkoani humo kusimamia agizo na kuhakikisha wanawasilisha michango yao kabla ya Juni 10, mwaka huu na atafurahi kuona Ndanda haipotezi nafasi ya kucheza Ligi Kuu Bara katika msimu ujao.

# Michezo

Jumamosi Juni 6, 2020

Nipashe




Chelsea yajipanga kumsajili Chilwell UKURASA 22



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa timu hiyo, Erasto Nyoni katika mazoezi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena hivi karibuni. **PICHA: SIMBA SC**

## Samatta awapa somo chipukizi

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI ndoto za wachezaji wengi wa hapa nchini na barani Afrika kwa ujumla zikiwa ni kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya, nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na mshambuliaji wa Aston Villa ya England, Mbwana Samatta, amewaondoa hofu na wasiwasi wa nyota hao ambao hawaifahamu vizuri lugha ya Kingereza.

Akizungumza na Nipashe jana, Samatta alisema kujua lugha hiyo maarufu si kigezo cha mchezaji kufanikiwa na amewataka kuendelea kujituma kwenye mazoezi ya kila siku.

Samatta alisema mchezaji anaweza kujifunza lugha hiyo kama sehemu ya kumrahisishia mawasiliano, lakini kamwe asifikiri hutumika wakati anafanyiwa majaribio.

"Kama bado kuna mchezaji mpira kinda anatoka Tanzania anafikiri kutokana na kutojua kwake lugha ya Kingereza kutamfanya ashindwe kucheza soka la kulipwa, basi aondoe huo wasiwasi kabisa, unaweza kujifunza kama nyongeza ya kurahisisha mawasiliano, lakini sio kigezo cha kufeli," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Mshambuliaji huyo alisema kokote duniani hakuna timu inayotumia kigezo cha lugha kumsajili mchezaji.

Aliongeza mchezaji mwenye uwezo mzuri hawezi kushindwa kukamilisha mchakato wa kusajiliwa na timu iliyoridhishwa na kiwango chake kwa sababu anashindwa kuzungumza kwa ufasaha Kingereza au lugha nyingine inayotakiwa na klabu husika.

# Yanga yatakiwa kujipanga

**Na Saada Akida**

### ●●●Ni kuelekea mchezo wao dhidi ya Mwadui, yaelezwa ikumbuke kilichoikuta Simba Kambarage...

TUMEJIPANGA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Mwadui FC ya Shinyanga, Khalid Adam, ambaye timu yake ni moja ya klabu ambazo zinapambana ili kuhakikisha zinabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Khalid alisema amewaongezea wachezaji wake programu maalumu ya mazoezi ili kuhakikisha wanaimarika na wanakuwa tayari kushinda 'vita' ya janga la kushuka daraja.**

Khalid alisema wamejipanga kuongeza umakini na kutumia vema uwanja wa nyumbani ikiwamo katika mchezo wao dhidi ya Yanga ambao utacheza Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM, Kambarage.

"Wachezaji wapo tayari kupambana kupata matokeo chanya na kujinasua katika nafasi mbaya ya kushuka daraja, tunataka kuanza na Yanga, wajipange," alisema kocha huyo ambaye alikuwa wa kwanza kuifunga Simba msimu huu akiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Alisema mikakati inaendelea vema na baada ya kuanza mazoezi ya pamoja, wachezaji wake wameimarika zaidi na sasa wako tayari kuanza kusaka pointi katika kila mechi watakayocheza.

"Kila kitu kipo sawa, ukizingatia tayari masuala ya michezo yameruhusiwa, tunasubiri kuona kwamba tunashinda mechi zetu zote, tunajua kuna ushindani mkubwa ila muhimu ni kupata matokeo mazuri kwanza kwenye uwanja wa nyumbani," alisema Khalid.

Kocha huyo alisema sasa wanajipanga kupata matokeo bila kujali timu wanayokutana nayo na wanazipa heshima timu zote watakazokutana nazo kwenye ligi hiyo.

"Tunafahamu na tunaelewe mechi yetu dhidi ya Yanga itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu hawatakuwa tayari kupoteza mchezo huo, ni mechi muhimu kwa kila timu hasa baada ya serikali kuruhusu kurejea michezo na tukiwa tumekaa nyumbani takribani miezi miwili kutokana na ugonjwa wa corona, tunawaambia waje na sisi tumejipanga," Khalid alisema.

Naye nahodha wa timu hiyo, Papy Tshishimbi, alimewataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kujipanga kuwapa 'sapoti' ili watimize malengo waliyonayo ya kuvuna pointi tatu katika kila mchezo.

Tshishimbi alisema ni jambo la msingi kwa mashabiki kuendelea kuipa sapoti timu yao hasa katika dakika hizi za lala salama.

"Tumejiandaa kurejea katika katika ubora wa kipekee, licha ya wachezaji tulikuwa nyumbani, lakini kila mmoja alikuwa anafanya mazoezi, kinachotakiwa kwa sasa ni mwendelezo wa sapoti yao ambayo ilikuwapo tangu zamani," Tshishimbi alisema.

Yanga yenye pointi 51, itashuka dimbani kuikabili Mwadui FC ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Namungo FC.

Katika kusaka makali, Yanga inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya KMC FC kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042